**102/2**
**LUGHA**
**KISWAHILI**
**USAHIHISHO**
**KARATASI 3**
**FASIHI YA KISWAHILI**
**OKT/NOV 2005**
**SAA 2 ½**

**(a) Katika shairi A**

- Sumu inalinganishwa na vitu vya bure yaani vitu vya kupewa ambavyo havikutolewa jasho.
- Wenye hekima hawavitaki vitu vya bure kwa sababu vina maudhi.
- Vya bure humwangamiza mtu akatupwa gerezani.
- Imefananishwa na tamaa ya mtu (tamaa mbaya) 5 x 1 = 5

**Katika shairi B**

- Matamshi ya binadamu yanaudhi ni sumu kali kuliko ya nyoka.
- Tamaa huzaa sumu.
- Anatumia maneno matamu yenye matokeo mabaya yanayoudhi.
- Urafiki umekuwa sumu inayowangamiza wengi
- Binadamu anadhulumu na wivu wa kisiri (nyoka itamwona lakini si binadamu)

2x 1 =2

(b)

- Cha bure japo hufanywa cha kuvutia au kitamu hatimaye kitakudhuru.
- Cha bure hata kama si kizuri au kitamu hulemasa juhudi.
- Budai ana furahia kikusabahi lakini ndani amejaa chuki/chungu/hapendi (unafiki)
- Mtu kama huyu kwako ni adui hujifanyi mtu mzuri lakini anataka kukuangamiza/adui. 4 x 1 = 4

SEGERA FESTUS'S SOFT COPY HUB: 0720121995

(c) Matatizo yaani giza ambalo linamgubiko mtu ili asifikiri (katika shairi A)

- Kufungukakiakili
- Matatizo/shida
- Kumtia mtu katika gereza la kawaida 1 x 2 = 2

Shairi B. Sehemu ambapo watu/wahalifu hufungwa, kwa hivyo tamaa huwesa kumfanya mtu aibe n.k. na kufungwa.

(d) Watu wenye hekima huwa hawana busara vitu vya bure na huviona vitu hivyo kama duni. Ni vitu ambavyo havipasi kumfaa binadamu bali wanyama kama vile tumbili/kima. Watu waungwana wastaambu huvibeza vitu vya bure. Vitu hivyo vinachukuliwa kama visivyostahili. 1x4 = 4

| (e) | **Shairi** 'A' | Shairi 'B' |
|---|---|---|
| | Taringia | Moyonimwe |
| | Kuendekeza | Kazidia |
| | Tamaaye | Aheri |
| | Siukabili | Atamani |
| | Teraje | |
| | Upuza | |
| | Takukwaruza | 2 x 1 = 2 |

(a) Hapati usingizi kwa sababu ya usumbufu wa jipu
Linamchoma kama sindano/kumpa uchungu
Limemwanza tangu zamani/tatizo ndogo lilikosa kushugulikiwa awali.
Liko makalioni hawezi kukaa/kuketi/daima anasimama.
Anaconda sababu ya j ipu.
Majuto/kutoshughulikia tatizo ndogo tangu awali.
Wayo wayo/mwako/kwajumla hana raha anaemia. 4 x 1 = 4

(b) - Anasubiri jipu Hive.

Atalitumbua jipu.

Uchungu hautamjalisha.

Atatengana na mateso ya jipu.

Ataunguza j eraha.

Atarudia afya yake.

Atarudia furaha yake. 4 x 1 = 4

(c) Ninajipu ambalo linampa taabu sana. Tangu liliponianza hilo jipu sipati usingizi mzuri. Ni mara yangu ya kwanza kuugua ugonjwa huu. Jipu lenyewe linanichoma kama sindano na uchungu wake ndio ninaoeleza. Alama 4

(d) - Nimekonda kama uzi

Latoma kama sindano

Kama ngombe alo nona

Kusimama; mtendeni - Balagha

} Tashbihi

1 x 1 =1

(e) - Hilo j ipu lilianza kama kipele

Hakujua kipele hicho kingekuwa jipu

Angalijua angejitafutia dawa kujitibu

Hakujua angetafuta suluhisho la tatizo mapema. 3 x 1 = 3

(f) (i) Wayowayo - hangaiko la moyo sababu ya usumbufu, kiwewe, wasiwasi, jaka moyo.

(ii) Kushtadi - kushamiri, kushika kani, kukazana, kukidhiri, kuzidi.

(iii) Idhilali - mateso, usumbufu, taabu, kutendekeza, sakawa, kero. 3 x 1 = 3

(g) (i) Kumfanya mvivu, baradhuli, mjinga, nyonge

(ii) Kulemeza na kukwamiza.

(iii) Hainipi radha nzuri, furaha, raha, hatimaye ni sumu.

(iv) Ingawa kinaonekana kizuri, kinaleta shida, matatizo ni sumu pia. Zozote

2 x 1 = 2

SEGERA FESTUS'S SOFT COPY HUB: 0720121995

**102/2**
**LUGHA**
**KISWAHILI**
**USAHIHISHO**
**KARATASI 3**
**FASIHI YA KISWAHILI**
**OKT/NOV 2006**
**SAA 2 ½**

**1.** **(a)**

- Ni silaha/kinga
- Ni ngome ya hishima/taadhima
- Ukweli huridhisha
- Ukweli hupatanisha *(4 x 1- = **alama** 4)*

(b) Stiari : Haki kuziangusha

- Tashhisi - Lakinga mbele na nyuma
- Tabdila -hifadha ***( 2 x 2 = alama**4)*

(c) Ilo - inkisari

Muongosha, kuhadaisha - tabdila

hishima- lahja _ ***(alama 4)***

(d) Ni haki kudanganya kwanza unapopatanisha,' pili unapotaka kuhifadhi ndoa au vitani. Katina miktadha mingine dumu katika ukweli. ***(alama 4)***

(e) (i) Kabisa ***(alama** 1)*

(ii) Ukiwa katika kesi tubu ama useme ukweli: Mola atakusaidia. ***(alama** 2)*

(iii)

- Wamewafanya wasadiki
- Wamewafanya waunge mkono ***(alama** 1)*

**2.** (a)

- Mkulima ambaye ni nguzo ya Afrika ni kama mturawa.
- Anateseka, ana huzuni na hana matumaini

SEGERA FESTUS'S SOFT COPY HUB: 0720121995

- Baadaye matumaini yanaweza kwisha
- Kuna siku ambapo atafahamu haki yake na aidai
- Wanaomtesa wataadhibiwa. ***(yoyote 4 x 1 = alama**4)*

(b) (i) Tashbihi

- Kama kuni
- Kama bahari

(ii) Kweli kinzani: Mtumwa wa watumwa waliyoridhiya

(iii) Tashhisi:

- Pumzi zilizozima taa za Afrika
- Amekita jembe lake akilisujudia ***(alama** 4)*

(c)

- Beti tano
- " Mishororo haitoshani
- Shairi hum
- Vina vya nje vipo ***( 3 x 1 = alama 3)***

(d) Mshangao, masikitiko kuwa aliye nguzo ya Afrika ni mtumwa wa watumwa

***(alama** 2)*

(e) (i) Wakati atakapozinduka na kuidai haki yake

(ii) Kutuliza hasira za matakwa/matatizo yake hata kama ni kidogo

*(2 **x 2 = alama** 4)*

(f) (i) Umbo

(ii) Uliokauka

(iii) kumwingisha/kumtopesha ***( 3 x 1 = alama** 3)*

**102/2**
**KISWAHILI**
**KARATASI 3**
**USAHIHISHO**
**FASIHI YA KISWAHILI**
**OKT/NOV 2007**
**SAA 2 ½**

**USHAIRI**

a). Msanii katika shairi hili anatuma ujumbe wa-kukomesha tohara ya wanawake kwa sababu athari zake ni mbaya kwa mwanamke. (alama 2)

b) i) Mwanamke hutaabika anapojifungua
ii)Tohara yaweza kuua mwanamke..
iii)Tohara hubeza hadhi ya mwanamke.
iv)Tohara -hudumiza fikra ya mwanamke (alama 2)

c) i) Takriri -Kurudiarudia maneno k.m tohara
ii) Istiari -Tohara ni kubwa sumu
iii) Tafsida -akijifungua badala ya akizaa

d) Kwa sababu ni utamaduni

e) Uelewe tohara ya siku hizi ni ugonjwa mkubwa unaomshika mwanamke na kumfanya akonde sana Tohara ya mwanamke asilari ikomeshwe, (alama 4)

f) (i) Adha -Jambo linalosumbua au kuleta shida/tabu/udhia.
(ii) Usimtimbe - Hali ya kumlazimishia mwanamke tohara. (alama 2)

g) i) Uhuru wa mwanamke
ii) Mwanamke kurithi mali kutoka kwa babake.
iii) Ndoa za mapema /lazima kwa wasichana. (alama 2)

SEGERA FESTUS'S SOFT COPY HUB: 0720121995

**KISWAHILI KARATASI YA TATU (3) 2008**
**MARKING SCHEME - LUGHA 102/3**

. **a).** i). wanajamii wanajishughulisha katiuka kazi mbalimbali ili kuboresha maisha yao lakini maisha yao ni duni
ii). vibarua (manamba, wachapakazi, mayaya, madobi, matopasi) wanaoajiriwa wanafanya kazi kwa bidii lakini mishahara yao ni duni
iii). viongozi serikalini wamepewa nyadhifa hizo za hadhi lakini hawajibiki kunyanyua hali za waliowachagua
iv). tabaka la chini ndio walio wengi katika jamii na ndio tegemeo la jamii lakini wanaishi maisha ya mateso mengi
v). haijulikani mateso ya walio wengi yatafika kikomo lini

zozote 4 x 1 = alama 4

).I) Kinaya
i). wasakatonge ndio wengi lakini hawana sauti
ii). makuli, mayaya, matopasi, wachapakazi n.k ni maskini
iii). wasakatonge wafanyao kazi kwa mateso mishahara yao ni duni
iv). wapelekao watu serikalini hawashughulikiwi na wahowachagua
v). Wazalishao mali hawana chochote bado ni maskini (manamba, madobi, mayaya, wachapakazi)

II) Taswira
i). wabeba zege ya marashani
ii). wasukuma mkokoteni
iii). makuli bandarini
iv). wachimbaji migodini
v). Manamba mashambani
vi). Wachapakazi viwandani
vii) matopasi wa majaani
viii) wanasiasa madarakani
ix) mayaya na madobi wa nyumbani
(siku zote wako matesoni)

III) Takriri
i ). wasokatonge
ii ). Juakali
iii). Lakini
iv). Wao
v ). Ni

). i). ulingunuzi/ ulinganushi
ii). wachimbaji migodini lakini maisha – yao ni ya chini
iii). wachapakazi viwandani lakini maskini

i). kipande kimoja
ii). shairi lina kituo/ kimalizio
iii). mizani hailingani katika kila ubeti
iv). beti 4

*SEGERA FESTUS'S SOFT COPY HUB: 0720121995*

v). mishororo 6 kila ubeti / tasdisa / usita au kila ubeti una kichwa au kijichwa / anwani na kila ubeti una mishororo mitano
vi). Mishororo wa kwanza vina vinabadilika ( li na – nge)
vii). Mishororo mitano ina vina vinavyofanana (ni)
viii). Mishororo wa kwanza katika kila ubeti unapindapinda ( pindu)
ix). Neno lakini limetumiwa mwanzo wa kila kituo – kikwamba

d). Watu wa tabaka la chini / ndio huwapa nyadhifa viongozi / kutokana na nyadhifa hizo viongozi hupata mali au uwezo wa kiuchumi / wale waliowachagua maisha yao ni ya kusikitisha

e). i). Kufanya kazi kwa bidii
ii). Kuwajibika – kwa umma katika kushiriki kuwachagua viongozi
iii). Viongozi wanastahili kuadilika kwa kunyanyua hali za umma na kujali hali Ya wafanyikazi

f). Manamba – vibarua, wafanyikazi
tabaka lisilo auheni – watu maskini / wasio na hali nzuri kiuchumi/ walalahoi

2) i). Maelezo ya sauti kuhusu uwezo mkubwa wa jua ambao mtemi hawezi kunyanyasa au kutesa. Uwezo wa jua unaashiria uwezo wa umma ambao utamwangamiza Bokono. Amekuwa ana uwezo wa kufanya mambo mengi lakini uwezo wa jua unaashiria kwamba umma una uwezo utakaomzidi Bokon na kumuongoa mamlakana
ii). Kutokuwepo kwa watu katika mkutano ni dalili kwamba watamuasi hatimaye. Watu hawakuwa na imani na uongozi wa Bokono kwani walikuwa wamechoswa nao
iii). Ndoto ya Bokono kuhusu kuzikwa kwake akiwa hai ni ishara ya kuangamizwa kwake na utawala wake. Ndoto inaonyesha dalili kuwa ingawa bokono angali hai wanabutangi hawamtaki
iv). Tendo la kushika mkia wa mjusi/ nyoka anayemuuma na kumwachia sumu ni ishara ya matokeo na hatari ya kuchezea haki za wananchi. Bokono kupuuza upinzani wa wanabutangi kwani haamini uongozi wake una hitilafu
v). Ndoto ya Tanya ya samba aliyelaa kando ya kisima ni ishara ya kiongozi anaywewazuia watu kufaidi rasilmali ya umma na uhuru. Bokono na uongozi wake umehodhi mali na kuwazua wanabutangi uhuru wa kufaidi nayo
vi). Ndoto ya pili ya Tanya kuhusu kichwa kinachobadili na kuwa na sura ya mwelusi ni mdokezo wa ishara ya mwelusi anayeuwa na nduguye Gege
viii) Masimulizi ya aski kuhusu kisa cha Makea aliyelelewa hoi na kuwa nusu maiti huku akichekelewa na jua ni ishara ya kiongozi anayepagawa na kulewa mamlaka anavyofanya Bokono Hatima ya uhai (maiti ya mjusi) inaashiria kikomo cha ungozi wa Bokono
ix). Nyalwe kutoa picha ya Bokono kurudi tumboni mwa mamake inaashiria mwisho wa utawala na Bokono

SEGERA FESTUS'S SOFT COPY HUB: 0720121995

**102/2**
**KISWAHILI**
**KARATASI 3**
**USAHIHISHO**
**FASIHI YA KISWAHILI**
**OKT/NOV 2009**
**SAA 2 ½**

(a) Maisha ya wafanyakazi na vibarua shambani ni duni na ilhali wanaofaidika ni wengine. ***(Alama** *2)*

(b) (i) Tabdila mvuwa, kibaruwa

Lahaja mte, kutipuza. mtilizi

Mazida —tisiya

Inkisari ikajinamiya/lingiapo

Kuboronga sarufi. Kutaja 1, mfano 1 zozote 2 x 2=4

(c) Tamathali:

i) Tashhisi - ndege walumbuizao

Uhaishaji/ Uhuishi - upepo uvumao kwa ghadhabu

Mito itiririkayo kwa furaha

ii) Ritifaa —— waulize ndege kwa nyimbo

—— iulize na mito

iii)Taswira —— maji itiririkao

—— upepo mkali kwa ghadhabu uvumao

iv)Takriri —— lulize, waulize, uulize

Kutaja alama 1 Kuelcza alama 1 Mbinu yoyote 1 x2 =2

**2. Mbinu ya kimuundo:**

**i)** Usambamba/Takriri —Urudiaji kimuundo

ii) Kina cha mwisho ni O/kipande 1

iii) Mizani ni sawa katika kila mshororo - 19

iv) Utatu/Tathlitha mishororo mitatu

*SEGERA FESTUS'S SOFT COPY HUB: 0720121995*

Mfana 1 Kutaja alama 1 Kueleza alama 1

*(alama 2)*

(d) i) Jasho la vibarua linafaidi wenginc

ii) Wale wanaonyonya vibarua wajue kwamba wanafanya liliiostahili.

iii) Vibarua wcnyewe wazinduke (mshairi anauli/a maswali ya kuchochea, ya kutafuta mwelekeo)

iv) Jamii nayo ijue vibarua wananyonywa.

v) Wanaotarajiwa kushughulikia haki /a vibarua hawajali

vi) Vibarua wanafanyishwa kazi nyingi kwa malipo duni

vii) Wanadharauliwa na kutukanwa. (Hoja zozote 2 x2=4)

(e) Swali ni kwamba ni nani anayelima na kupalilia masharnba? Mimea inayopatikana kwa wingi shambani ika/aa kwa wingi kutokana na juhudia mkulima ambaye ni kibarua. Mwishowc ni nani anayepata utajiri wa mali hiyo yote akajilimbikizia, akanona na kuwa kama ana mimba hata akaongc/,a magari na kujipatia starehe kama kuwabadilisha wanawake. Swali hili liuli/Avc iii kubainisha ni nani hasa anayefanya kai hiyo. (alama 4)

(f) Kibarua manamba ni jina la :

i) tajiri au mwenye shamba

ii) mfanyikazi shambani (Tazama matumizi ya herufi kubwa) *(1x2 = 3)*

(a) Hiki ni kipera cha fasihi simulixi kinachohusisha mazungumzo yenyc Iengo la kuhimiza mwelekeo na tabia zinazokubalika katika jamii.

(b) **<u>Muundo wa mawaidha</u>**

Mawaidha yanaweza kujisimamia au yakaegemezwa kwenye utanzu mwingine kama utambaji. Yakiwa yamejisimamia, muundo wake utakuwa ufuatao:
(kuitayarisha hadhira
kujua nini kunachofuata)

Utangiulizi: Hapa anaycloa mawaidha huan/a kwa kutoa kauli za kivutia nadhari za hadhira yake 'km "Naomba mnisikiHze kwa makini nk

Uvulajawa nadhari unaweza kuhusisha utoaji \va kiini cha mawaidha hayo km "Ni muhimu k\va kiia kijana na mwanajamii kujua wajibu wake.

- **<u>Mwendelezo/lJwasilishaji</u>**

Katika sehemu hii mtoa mawaidha hukazia lengo la mawaidha yake kwa kutumia mambo kama vile udondoaji wa semi au kauli za watu maarufu kalika jamii. Lugha fasaha na yenye vinawirisho, viziada lugha, mabadiliko ya kasi ya mazungumzo,

kupanda na kushuka kwa sauti, kimya nk. Mtoa mawaidha huusia, huonya, buelimisha kutcgemca iengo la mawaidha yake.

- **<u>Hitimisho</u>**

i) Mwasilishaji:Aghalabu katika sehemu hii mtoa mawaidha hushirikisha hadhira yake kwa kutaka kusikia msimamo wao kuhusu mawaidha yake.
Mali kadhalika humtaka kila mmoja kuehukua hatua.
Anaweza kuwaomba kueleza ni hatua gani watachukua au kuwasisisitizia umuhimu wa kuehukua hatua huku akitumaini kuwa kila mmoja atafan>'a liivyo.

ii) Iladhira maoni yao, mapendekezo yao, changamoto. (4x1= 4)

(c) Sifa za mawaidha

i) Huhusisha kundi maalum la wanajamii (watoaji wapokeaji)
ii) Aghalabu mawaidha hutolewa na wazee wanaoehukuliwa kuwa na hekima
iii) Hutolewa kwa wadogo, vijana au watu wanaohitaji ushauri
iv) Watoa mawaidha hutarajiwa kuwa watu wenye haiba, heshima , waadilifu, wajuzi wa mambo na wenye tajriba kuu katika maisha.
v) Hutolewa katika mikutadha i,id.alum aghalabu katika hafla/shcrchc/miviga, arusi, vikao vya jamaa/familia au pahala popote ambapo yanahitajika.
vi) Tamathali za semi zinazaovuta nadhari hutumika kwa w ingi.
vii) Hutumia lugha ya kipekee inayoshirikisha maneno yenye maana n/ito na inayolenga kuathiri wanaousiwa.
viii) Huweza kugusia mambo mengi maishani kama vile elimu, rasilmali, maadili, urithi, mapenzi na unyumba, dini, kifo, malezi, uongozi nk.
x) hutofautiana kutengemea jinsia ina\rohusika. Mawaidha yana\rotolewa kwa Wavulana huweza kuwa tofauli na vale yanayotolewa kwa wasiehana.
x) Viziada lugha kama vile kupanda na kushuka kwa sauti, miondoko na viungo n.k hutumika kwa wingi.
xi) Huweza kufungamanishwa na \risa maalum vilivyotokea katika jamii kusistiza ujumbe.

(Zozote 7x2 = alama 14)

**102/2**
**KISWAHILI**
**KARATASI 3**
**USAHIHISHO**
**FASIHI YA KISWAHILI**
**OKT/NOV 2010**
**SAA 2 ½**

**1.** (a) -Kufungwa

-Kunyimwa uhuru

-Alipofimgwa pameharibika

-Angependa kuhama lakini hawezi

-Kuna majani mengi mbele yake lakini hawezi kuyafikia zozote 4 x 1 =4

(b) - amekwisha zoea hali yaki

-Hapendi kuonekana tofauti. Hataki kuukosa utu kwa sababu amefungwa katika kamba ya utu. 2 x 1-2

(c) Ni dhamiri katika nafsi yake ambayo ameshikilia ambayo haionekani kwa macho ndiyo iliyomfunga (alama 2)

(d) (i) -Tashbihi -kama mbuzi

-Kama mbwa

(ii) Istiari/sitiari -Sahani ya mbingu, kamba isiyoonekana

Kutaja- 1 Kutoa mfano

(iii) Tasfida- Nimekwishapachafua Zozote 2 x 2=4

(e) Mishata: Mishororo ambayo maana yake inakamilika katika mshororo unaofuata

Mf: Kami kwa mbaya bahati, katika uhuru kupigania kamba ni fupi na nimekwishachora duara.

Kami kwa mbaya bahati, katika
Uhuru kupigania, Sahani ya mbingu
Nimeipiga teke na niigusapo kwa mdomo
Mbali zaidi inakwenda na siwezi tena
Nami sasa sitaki ikatike maana
Mbuzi wa kamba alipofunguliwa, mashamba

SEGERA FESTUS'S SOFT COPY HUB: 0720121995

(f) Nimefungwa kama rnbwa na kwa bahati mbaya katika kutaka kuondoka pale nimeipiga teke sahani ya mbingu ambayo imeenda mbele na siwezi kuifikia. Na pale nilipofungwa ni pachafu ila siwezi kupatoka.

. **2.** Mtahiniwa anahitajika kuonyesha kufanana kwa vipera hivi na vile vile kutofautiana kwake.

**Majibu**

**Kufanana**

(i) Vyote ni vipera vya semi katika fasihi simulizi

(ii) Zote ni kauli fupifupi ambazo hutoa ujumbe kwa kutumia taswira au picha
Km kitendawili nyumba yangu haina mlongo
Hapa tunaingiwa na taswira ya nyumba isiyo na mlango
Methali: Mtoto akibebwa, hutazama kisogo cha mamake
Inapotajwa methali hii, tunaona picha ya mtoto aliyebebwa akitazama kisogo cha mamake

(iii) Vyote huweza kutumia lugha ya mafumbo km kitendawili
Methali: Uvivu ni nyumba ya ajizi.

(iv) Vyote huchota kutoka mazingira au jamii husika. Hutumika kutekeleza Majukumu yanayofanana. Mathalan vyote hutumika kuelimisha wanajamii, kuburudisha na pia kuendeleza utamaduni wa amii. zozote 5 x 2=10

**Tofauti**

i. Aghalabu methali huwa na muundo wenye vipande viwili. Kipande cha kwanza huwa ni kauli ambayo hukamilishwa na kipande cha pili. Km Fahali wawili wapiganapo, nyasi ndizi huumia.

ii. Methali huwa ni kauli nzito ambazo mara nyingi hazibadilikibadiliki.

iii. Methali huweza kutumia tamathali nyingi za lugha kuliko vitendawili;

Km. Waweza kutumia tashihisi km Chui naye ana mke pia
Takriri: Habanahaba, hujazakibaba.

iv. Kimaudhui, methali huwa na maana ya juu juu na maana ya ndaniVitendawili huwa na maana hiyo moja.

v. Vitendawili huwa na fornula maalum ya uwasilishaji. Pana anayetega na anayetakiwa kutegua.

vi. Vitendawili hubadilika badilika kutegemea mazingira au mpito wa wakati

vii. Dhima ya vitendawili si pana sana kama ya methali.

viii. Methali huhusisha mtu mmoja lakini vitendawili huhusisha wawili au zaidi.

zozote 5 x 2 = 10

**102/2**
**KISWAHILI**
**KARATASI 3**
**USAHIHISHO**
**FASIHI YA KISWAHILI**
**OKT/NOV 2011**
**SAA 2 ½**

1. (a(i) Haya ni maelezo ya mwandishi kuhusu mawazo ya selume katika ndoa.

(ii) Anahisi hana mume kwani shoka amepuuza wajibu wake/ mzohali

(iii) Amemwachia jukumu la malezi na kutafuta riziki, kazi ya Shoka ni kudoea alichotafuta selume.

(iv) Kama si wanawe Selume hangejisumbua kutafuta chakula

Zozote (4 x 1 = 4)

(b)

(i) Sitiara/ jazanda (1 x 1 = 1)

Mfano: Shimiri za baruti (1 x 1 = 1)

Maalezo: Matatizo ya ndoa (1 x 2 = 2)

(ii) Msemo/ Nahau: kutanga na njia – kuhangaika, kutafuta

(iii) Nida/ siyahi: Lo- kuonyesha hisia za kuchukizwa na mkondo wa ndoa yake.

(c)

(i) Kudhulumiwa kwa mwanamke katika ndoa km. Selume na shoka

(ii) Kutowajibika kwa wanaume. Km Shoka

(iii) Wanawake kuendelea kubaki katika ndoa zenye matatizo kwa sababu ya watoto wao na kujitolea katika yaliyopuuzwa na waume wao.

Zozote 2 x 2 = 4 ( Mwanafunzi arejeree mifano kitabuni)

(d) (i) **Asasi ya ndoa/ unyumba – ndoa ya maksuudi na tamima naya maksuudi na mwanasururu**.

(i) Matatizo kati ya mume n mke

(ii) Dhiki zinazowakumba wanawake katika ndoa

SEGERA FESTUS'S SOFT COPY HUB: 0720121995

(iii) Tamima analazimika kutawa kwa amri ya mumewe Bw. Maksuudi

(iv) Hana ruhusa ya kutoka wala kumwalika mtu nyumbani.

(v) Analazimika kujifungua nyumbani licha ya ushauri wa madaktari kutokana na kufukuzwa nyumbani.

(vi) Ananyimwa uhuru wa kuwa na mwanawe mdogo anayeishia kufariki

(vii) Tabia ya Bw. Maksuudi inaishia kuivunja jamaa yao.

(viii) Bw. Maksuudi anamwacha mkewe na kuwafuata wanawake wengine huko nje

(ix) Mwanamke ananyimwa uhuru wa kuishi kama kiumbe anaweza kujiamlia

(x) Mwanamke hana uhuru wa kiuchumi. Km Mwanasururu ananyimwa urithi wake.

2. **Utengamano wa kijinsia/ taasubi ya kiume/ utengano kati ya wanawake na wanaume/ mgogoro wa kijinsia**

(i) Wanawake wanatumiwa kama vyombo vya starehe km. kazija na maksuudi, shoka na mainmuna.

(ii) Uhusiano kati ya mwanamke na mwanaume unatawaliwa na chuki na kisasa – Biti. Kocho/ Farashuu na maksuudi, kazija na maksudi.

(iii) Tamina anateswa na maksuudi hataki kumsamehe na kumrudia anapomtaka kufanya hivyo.

(iv) Uhusiano wa Maimuna na Bw. Maksuudi babake unaonyesha chuki inayotokana na matendo ya maksuudi mwenyewe.

(v) Kazija anapanga njama ya kumfumanisha maksuudi na mwanawe Musa.

3. **<u>Ukatii</u>**

(i) Maksuudi anavyomtrnda Bi. Tamina

(ii) Maksuudi anavyomtenda mwanasururu

(iii) Maksuudi kumpiga na kumfukuza/ taliki Bi. Tamina ilhali ana tumbo bichi

4. **<u>Dhiki/ kudhulumiwa kwa wanawake</u>**

(i) Maksuudi kutawisha Bi. Tamina na Maimuna

(ii) Maksuudi kumwendea kinyume Bi. Tamina ( Jicho la nje)

(iii) Maksuudi kumpora Mwanasururu mali yake

(iv) Wanawake kuachwa nyuma kielimu na kikazi

5. **Nafasi mwanamke katika jamii**

(i) Wanawake kujihusisha na ukahaba ili kujikimu

(ii) Wahusika wengine waliishi maisha katika makazi duni km. Farashuu, Maimuna, Mwanasururu.

6. **Umaskini**

(i) Wanawake kujihisisha na ukahaba ili kujikimu

(ii) Wahusika wengine waliishi maisha katika makazi duni km Farashuu, Maimuna, Mwanasururu.

Kutaja – 1,Maelezo – 3,Maudhui yoyote – 2,Jumla – 8

2. (a) Maisha ya wafanyakazi na vibarua shambani ni duni na ilhali wanaofaidika ni wengine ( al. 2)

(b) (i) Tabdila- mvuwa, kibarua, tisiya

(ii) Lahaja – mte, kutipuza, mtilizi

(iii) Mazida- tisiya

(iv) Inkisari – ikijinamiya, lingiapo

(v) Kuboronga sarufi – uuliza na upepo ( mfano wowotw ufaao)

Kutaja – 1 Mfano – 1 ( Zozote 2 x 2 = 4)

(c) (i) Tamathali za usemi

(ii) Tahishishi/ uhuishi – ndege watambuizao, upepo uvumao kwa ghadhabu, mito itiririkayo kwa furaha

(iii) Taswira – maji itiririkao, upepo mkali wa ghadhabu uvumao

(iv) Takriri/ uradidi- waulize, iulize, uulize

Kutaja – 1 Kueleza – 1

**102/2**
**KISWAHILI**
**USAHIHISHO**
**KARATASI 3**
**FASIHI YA KISWAHILI**
**OKT/NOV 2012**
**SAA 2 ½**

**1.** (a) - Ni safari ya kupigania uhuru/ safari ya kutafuta haki/ safari au harakati za kujiendeleza kiuchumi. Anasema walishikana kwenye safari ya haki, walisita kwenye mlima wa haki. Anataja kuteremsha miliki,

Kutaja - alama 1 Kueleza - alama 1

(b) Maelezo ya (maana ya) kinaya yawepo.

- Kinyume cha matarajio, (viongozi) wachache waliofika kileleni walijawa na uchoyo, wakaamua kujinufaisha. (alama 1)
- Walijitengenezea makazi ya raha, wakajinyakulia vyeo wakakaa kufurahika/huku wakiwasahau waliowakweza mamlakani.
- Wakawa ndio pekee waliofaidi matunda ya uhuru ambayo yalikuwa yamepiganiwa na wote.
- Viongozi wamefika hadi kuwadhuru raia waliowapa hivyo vyeo - wanawatemea mate.
- Raia kupigania uhuru na baadaye kutofaidika kwao.
- Kutofikia maazimio ya kiuchumi. Hawapati milki waliopigania
- Safari ya haki na hali ubaguzi unajitokeza.

(5 x 1 = alama 5)

(- kueleza kinaya/ kujitokeza kwa kinaya - alama 1)

Jumla - 6

(c) (i) Msuko - Mshororo wa mwisho una mizani chache kuliko mingine/ umefupishawa.

(ii) Ukara - Vina vya kati/ ndani vinabadilikabadilika. Vya nje/ mwisho vinatiririka.

(2 x 2 = alama 4)

(Kutaja - I, Kueleza -1)

(d) Mfano:

Wawakilishi/viongozi walijikuta katika hali nzuri sana za maisha na tamaa ya kujinufaisha ikazidi. Walishiriki starehe za kila aina. Katika hali hii walisahau

SEGERA FESTUS'S SOFT COPY HUB: 0720121995

wananchi/ raia waliowakweza katika nafasi hizo (waliowapa nafasi hizo) za uongozi, na ambao ndio waliokuwa na nyenzo za kuwafanya kufikia hali hii yao (viongozi) ya sasa.

(alama 4)

(e) - Inkisari tukawa'chia - kutosheleza idadi ya mizani.
- Kufinyanga sarufi/kuboronga sarufi/kubanaanga lugha/miundo ngeu ya kisintaksia.
- Kialeni wadiriki - wadiriki kileleni - kuleta urari wa vina.
- Tabdila - shaki - badala ya shake - kuleta urari wa vina.
- Lugha chakavu/msamiati
kikale, - Kialeni - Kileleni
- Kulipa shairi mapigo ya kimuziki
- Kulipa shairi upeke wa kiutanza.

(kutaja - alama 1, maelezo; alama 1) ( $2 \times 2$ = alama 4)

**2.** (a) (i) Maana ya Kijujuu.
-Nichaiyajioni.
- Inanywewa na mume na mke huku wakiwatazama watoto wakicheza .
- Chai inakaribia kumalizika.
- Mzungumzaji anamtaka mwenzake wahakikishe warneviacba vikorabe vyao vikiwa safi. ( $3 \times 1$ = alama 3)

(ii) Maana ya kitamathali.
- Shairi ni sitiari ya maisha yao ambayo yanakaribia kumalizika. Wameanza kuzeeka.
- Bembea - Sitiari ya maisha yao ya ndoa/ safari yao ya maisha/ chai ya jioni (Ushirika/uwepo wao katika siku za mwisho au maisha yanavyokaribia kuisha.
- Waliyopitia katika maisha yao ya ndoa - chamgamoto na furaha (kulikuwa na wakati lipokudaka ulipokaribia kuanguka).
- Maazimio ambayo hawakufikia - (sasa tukisubiri ndoto tusizoweza kuzitekeleza tena.
- Mume/ mke anamtaka wamalizie siku zilizobaki vyema.

SEGERA FESTUS'S SOFT COPY HUB: 0720121995

- Anamkumbusha siku walipokutana mara ya kwanza wakijaribu kujenga urafiki/ kuchumbiana. (3 x 1 = alama 3)

(b) (i) Usimulizi.

- Nafsineni inasimulia wakati walipokuwa wakicheza bembea/jinsi walivyofurahia rnaisha pamoja kwa matuniaini.
- Anasimulia siku walipokutana.

Mfano - 1 x 2 (alama

(ii) Usambamba.

Huu ni urudiaji wa muundo sawa/ huo huo wa mshororo/sentensi.

Mfano:

- kulikuwa na wakati ulinisukuma juu.
- kulikuwa na wakati nilikudaka.

Mifano -2x1 (alama 2)

(iii) Taswira

- Pana picha ya watu wanaokunywa chai na watoto wanaocheza bembea.
- Picha ya wenzi wa ndoa wenye furaha/wenye ushirikiano/wanaoongozana jikoni kupika.
- Picha ya watu wakitafuta tawi la kufungia bembea, na mbwa akiwasubiri.
- Picha ya nafsineni/mshirika katika ndoa anayemwambia mwenzake (kwa masikitiko) maisha yao karibu yanafikia kikomo.

Mifano -2x1 (alama 2)

(c) Nafsineni - ni mzuugumzaji au msimulizi katika kazi ya kifasihi. Nafsineni katika shairi hili ni mwenzi katika ndoa (mume au mke). Anasimulia walivyokutana, anataja watoto wao.

(kutaja - 1,
Kueleza - 1)
(alama 2)

(d) - Toni ya mchanganyiko wa furaha matumaini na raasikitiko/huzuni (alama 1)

Mifano: (i) Mzungumzaji anasimulia maisha yao ya furaha; kucheza bembea, kupika pamoja...

(ii) Hata hivyo anaonyesha hay a karibu yatafikia kikomo, anasema wamalizie chai yao yajioni.

(iii) Kuna maazimio yasiyofikiwa - anasema wanasubiri ndoto wasizoweza kuzitekeleza tena.

(iv) Anakumbuka kwa furaha na masikitiko siku yao ya kwanza kukutana.

(v) Ana matumaini ya kumalizia machicha (masalio) ya chai yao. (3x1= alama 3)

(e) - Kutenda mema
- Kurekebisha yaliyo kombo katika maisha/ uhusiano wao na wanajamii wenzao uwe wa kuridhisha.
- Kukamilisha/ kutimiza waliyoazimia kutimiza. (Hoja 1x2 = alama 2)

**3.** (a) - Nyimbo huhifadhi historia ya jamii, kwa mfano, nyimbo za sifa, nyimbo za siasa, nyimbo za vita.
- Huhifadhi na kupitisha utamaduni k.v. mbolezi hubeba utamaduni wa jamii kuhusu kifo,mazishi.
- Kuliwaza - k.v. mbolezi.
- Kuonyesha ustadi/ ubora wa jamii - wimbo bora/ mwema huonyesha ubora wa msanii.
- Kuhamasisha, kwa mfano nyimbo za kisiasa huhamasisha kupinga udhalimu.
- Kuelimisha - nyimbo za kazi (hodiya) hufunza maarifa ya kazi kama vile ukulima na usasi.
- Hukuza utangamano - Nyimbo za kazi, warn wanapoimba pamoja hujihisi kuwa kundi moja.
- Ni njia ya kutakasa hisia. Nyimbo za mapenzi na mbolezi hutumiwa kutoa hisia za moyoni.
- Huadilisha - Nyimbo hufumbata maadili ya kijamii na kidini. Kwa mfano nyimbo za kidini, bembelezi na hata mbolezi.
- Kukashifu tabia hasi - K.v. nyimbo za jandoni (nyiso) kukashifu woga.
- Kusifu tabia chang - K,v, sito
- Hukuza uzalendo - Wimbo wa taifa, nyimbo za kisiasa/huhimiza raia kujitoa mhanga kwa nchi.
- Kuimarisha ubunifu - Kadiri mtu anavyoimba ndivyo anavyonoa stadi za utunzi na uimbaji.
- Ni nyenzo ya burudani. Takriban aina zote za nyimbo hulenga kuburudisha tumbui zo.
- Hurithisha sanaa yenyewe ya uimbaji na utunzi wa nyimbo kwa vizazi kwa kuziimba kutoka kizazi hadi kingine.
- Hutumiwa katika vipera vingine kama vile ngano kuhuisha hadhira.
(5x2 = alama 10)

**Tanbihi**

Mtahiniwa <u>sharti</u> atoe mifano ya aina za nyimbo zinazotekeleza majukumu aliyotaja.

(g) Illi kufanikisha uwasilishaji wa wimbo, mwimbaji anahitaji:
- kuwa na sauti ya kuvutia ili kuvuta makini ya hadhira/kuiwezesha hadhira kupata ujumbe, kuihuisha kupata ujumbe.

SEGERA FESTUS'S SOFT COPY HUB: 0720121995

- kuihusisha hadhira, kwa mfano, kupitia kwa kupiga makofl ili kukinga dhidi ya ukinaifu.
- kutumia udramatishaji/ uigizaji ill kusisitiza ujumbe/ kuufanya wimbo kuvutia/ kuifanya hadhira kukumbuka.
- kuelewa hadhira ili kuubuni wimbo upya/ kutumia mtindo ufaao kuuwasilisha.
- kuuelewa utamaduni wa hadhira ili kukinga dhidi ya kutumia maneno/ishara zinazokinzana na utamaduni huo.
- Kutumia viziada lugha kama vile ishara za uso na kidatu kusisitiza ujumbe.

- Awe mkakamavu ili awasilishe wimbo bila kuogopa hata kama unashirikisha masuala ambayo ni mwiko/nyeti.
- Aelewe lugha ya hadhira ili aweze kuitumia kufanikisha uimbaji wake.
- Awe mbunifu wa kuweza kuubuni wimbo upya kulingana na hadhira. Wimbo wa watoto uhusishe nyenzo kama vile mchezo wa sauti na maneno.
- Awe mfaraguzi ili kuuimba wimbo kwa mahadhi tofauti tofauti ili adumishe mvuto.
- Ahusishe masuala ibuka/ masuala yanayoiathiri jamii wakati huo ili kupitisha maadili yafaayo.
- Awe na kumbukumbu nzuri ili aweze kuzirithisha nyimbo kama alivyoimbiwa (kifani na kimandhui) bila kubadilisha sana.
- Avae maleba yanayoafikiana na wimbo anaowasilisha ili kurahisisha uelewa wa ujumbe.
- Abadilishe toni kulingana na ujumbe anaopitisha ili kuibua taathira ifaayo kwa msikilizaji.
- Kutumia ala kwa njia mwafaka ili kukuza mvuto wa utungo wake.

**Tanbihi**

Mtahiniwa <u>lazima</u> atoe ufafanuzi toshelevu/unaoridhisha ili kutuzwa alama 2 kwa hoja.

(5x2 = alama 10)

**102/2**
**KISWAHILI**
**USAHIHISHO**
**KARATASI 3**
**FASIHI YA KISWAHILI**
**OKT/NOV 2013**
**SAA 2 ½**

**FASIHI SIMULIZI**

(a) **Maana ya Vitanza Ndimi**

Vitanza ndimi ni virai/vishazi au sentensi zenye sauti zinazokaribiana au zinazofanana kimatamshi na ambazo hutatiza mtu kuzitamka. Aghalabu huundwa kwa vitate, vitawe, au hata kurudia maneno yale yale katika sentensi. Kwa mfano:

(i) Wali huliwa na mwana wa liwali. Asiyekuwa mwana wa liwali hali wali.
(ii) Wali huliwa na wanawali, wasio wanawali hawali wali.
(iii) Shirika la reli la Rwanda lililiathiri lile la reli la Kenya.
(iv) Mzee aliyevaa koti lililofika gotini alianguka akaumia goti kisha koti Lake Lenye kufika magotini likachanika.

(alama 2)

(b) **Majukumu ya Vitanza ndimi**

(i) Kumzoesha mtoto/mtu kuzitamka sauti au maneno vizuri.
(ii) Ni nyenzo ya burudani. Vikao vya mashindano ya utamkaji hutumiwa kuwachangamsha wanajamii.
(iii) Msingi wa kumsaidia mtoto kujua lugha kwa undani. Huundwa kwa vitate Au vitawe, hivyo mtu hujifunza vipengele hivi vya lugha.
(iv) Husaidia kuimarisha uwezo wa kimawasiliano wa anayehusika. Utamkaji wa vitanza ndimi kwa kasi humzoesha mzungumzaji kuweza kuwasilisha hoja bila kusitasita.
(v) Huendeleza utamaduni. Jinsi wanajamii wanavyoshirikishwa katika utamkaji ndivyo wanavyorithishwa utamaduni wao au desturi yenyewe ya kushiriki katika utamkaji.
(vi) Hujenga stadi ya ukakamavu. Kadiri mtu anavyoshiriki katika utamkaji ndivyo anavyoimarisha ujasiri wake wa kuzungumza hadharani.
(vii) Huibua ucheshi na kudumisha uhusiano mwema. Utani unaoibuliwa katika mashindano ya utamkaji ni msingi wa kujenga uhusiano.
(viii) Hukuza ubunifu. Wanajamii huweza kubuni vitanza ndimi hapohapo, wakavitamka.
(ix) Ni kitambulisho cha jamii. Kila jamii ina vitanza ndimi vyake vinavyohusu mazingira yake.

SEGERA FESTUS'S SOFT COPY HUB: 0720121995

(x) Hukuza utangamano katika jamii. Vikao vya mashindano ya utamkaji huwaleta wanajamii pamoja hivyo kujihisi kuwa kundi moja.

(xi) Kuonya/kushauri - baadhi hufumbata maonyo/ushauri. Kwa mfano, Mzaha mzaha huzaa usaha. (6 x 1 = 6)

Kutaja ½ Mfano ½

(c) (i) Utazamaji wa kushiriki au kutoshiriki. Mtu anaweza kushiriki katika kikao cha utamkaji wa vitanza ndimi, hivyo kujua vinavyoendelezwa katika jamii husika.

(ii) Video. Mtu anaweza kupiga picha za video watu wakitamka/wakishindana katika. utamkaji wa vitanza ndimi ili kuja kuchanganua baadaye.

(iii) Matumizi ya hojaji. Mtu anaweza kuandaa maswali katika hojaji ili kudadisi kwa mfano, kama vipo katika jamii fulani, wanaohusika katika vikao vya utamkaji na uundaji wake.

(iv) Kurekodi kimaandishi (kuandika) ili kuvirithisha au hata kuvichanganua baadaye.

(v) Majadiliano ya vikundi lengwa, Mtafiti anaweza kuteua vikundi, kwa mfano, vijana, ili kuchunguza namna wanavyoviunda na kuvitamka, na athari ya vitanza ndimi hivi kwao.

(vi) Mahojiano Mtafiti anaweza kuandaa mahojiano rasmi na kundi / sampuli lengwa ili kuchunguza kwa mfano, majukumu ya vitanza ndimi katika jamii husika

(vii) Matumizi ya vinasa sauti na sidii ili kunasa utamkaji wenyewe na kuchanganua sifa zake.

(viii) Kutumia kumbukumbu ya mtafiti mwenyewe. Utafiti ambaye in mmoja wapo wa wanajamii katika eneo analofanyia utafiti anaweza kurithisha yale anayokumbuka baada ya kuyashuhudia.

(ix) Kusoma majarida na vitabu (maktabani) vyenye habari kuhusu vitanza ndimi.

(6 x 2 = 12)

**Tanbihi**

Hoja zifafanuliwe ili kupata alama kamili.

***Mstahiki Meya: T. Arege***

4. (i) Badala ya Wanacheneo kutafuta suluhisho kwa matatizo yao wanadai kwamba nchi ni
maskini. Waridi anamwambia Siki kwamba nchi ni maskini ombaomba, ndivyo wanavyoambiwa na vyombo vya habari, wasomi na wanasiasa.

SEGERA FESTUS'S SOFT COPY HUB: 0720121995

(ii) Badala ya Meya kushughulikia matatizo ya Wanacheneo, anasema Cheneo ni kisiwa cha kupigiwa mfano. Anajifananisha na majirani dhaifu kiuchumi na kukosa kuiendeleza Cheneo zaidi.

(iii) Meya anaupujua uongozi wa Cheneo kwa kuwaacha washauri wapotoshi kuuingilia. Anamhusisha Bili katika maamuzi muhimu kama vile utoaji wa kandarasi na hali Bili si mtaalamu katika masuala haya.

(iv) Meya anaifilisi Cheneo kwa kuidhinisha malipo yasiyofaa kama vile nyongeza ya mshahara wa madiwani, na malipo kwa Bili kwa kutoa ushauri ambao kwa kweli unahusu wizi wa fimbo ya Meya.

(v) Viongozi wa kidini kama vile Mhubiri wanachangia katika kudhoofika kwa uongozi wa kisiasa kwa kutomshauri Meya vyema. Anamwombea Meya ili naye (Mhubiri) afaidike kwa sadaka anayoidhinisha Meya.

(vi) Viongozi wanaufisidi uchumi kwa kutotekeleza malengo ya kimaendeleo. Meya anasema yeye anazingatia maazimio ya kimilenia ambayo kwa kweli hayashughulikii; watoto bado wanakufa kwa magonjwa yanayotokana na ukosefu wa lishe.

(vii) Viongozi wanawaachia wageni kuingilia masuala ya kiuchumi. Maamuzi muhimu kama vile kugawana kwa gharama ya matibabu yanatolewa na wageni na kuwafanya raia wateseke.

(viii) Meya anaifanya jamii ya Cheneo kuwa tegemezi kwa misaada. Anahofia kwamba hali ya usafi ikizorota wafadhili hawatakuja.

(ix) Viongozi wanaufifilisha uchumi kwa ubadhirifu wao. Meya anatumia pesa za ufadhili kununulia mvinyo kutoka ng'ambo badala ya kuanzishia miradi.

(x) Meya anapunguza kodi ya mapato ya Baraza kwa kuidhinisha kutolipa kodi kwa madiwani. Kupuuza malalamishi ya wafanyakazi kunasababisha kutokusanywa kwa pesa, hivyo kuliteteresha pato la Baraza.

(xi) Wafanyakazi kama vile Waridi wanajiuzulu wanapoona hali ni mbaya badala ya kukabiliana nayo.

SEGERA FESTUS'S SOFT COPY HUB: 0720121995

(xii) Viongozi wanashindwa kuwahakikishia raia usalama wa chakula. Mama anamlisha mwanawe wali na maharagwe yaliyolala na kusababisha kifo. Anasema wanakula chakula cha mbwa.

(xiii) Wanataaluma wanajiepusha na siasa, hivyo kutochangia kuiboresha siasa (mfano Siki).

(xiv) Kumpa Meya mamlaka makubwa kunachangia kupalilia udikteta badala ya demokrasia.

(xv) Kutoshughulikia afya ya kijamii kunasababisha magonjwa kama vile utapiamlo yanayotokana na ukosefu wa lishe.Waridi anashangaa vipi mama anawaletea mtoto mwenye ugonjwa wa utapiamlo; kwake hili ni jambo dogo.

(xvi) Badala ya raia kuimarisha viwango vya elimu na huduma za afya, wanawapeleka jamaa zao ng'ambo kwa huduma hizi. Meya analalamikia elimu duni, anampeleka mwanawe kusomea ng'ambo. Anampeleka mkewe kuzalia ng'ambo. Kwa njia hii anaujenga uchumi wa nchi husika na kuuibia ule wa Cheneo.

(xvii) Meya analiibia baraza na kuufisidi uchumi wake kupitia kwa kandarasi. Pia anaidhinisha wizi wa fimbo ya Meya/ardhi.

(xviii) Askari wanazorotesha amani na usalama wa raia. Wanawahangaisha raia kwa bunduki na vitoa machozi.

(xix) Viongozi wanasababisha kuzorota kwa hali ya usafi Cheneo kwa kutoshughulikia malalamishi ya wafanyakazi. Hili linaileteа Cheneo aibu na kuiumbua machoni mwa jamii ya kimataifa. Wageni wanaahirisha ziara yao. Mji umejaa uvundo unaohisika hata nyumbani mwa Meya.

(xx) Watu wanawachagua viongozi licha ya kujua kuwa viongozi hao wamekosa uwajibikaji, hivyo kuzizorotesha siasa za nchi/kuuzorotesha uongozi wa kisiasa.

(xxi) Meya anauangamiza uongozi wake mwenyewe kwa kupuuza ushauri wa Diwani wa III na Siki.

(xxii) Mapuuza ya Meya yanapalilia ukosefu wa utulivu kupitia kwa migomo ya wafanyakazi.

(xxiii) Meya analifilisha Baraza kwa kulipagaza deni. Bili anamshawishi amwambie mwanakandarasi alishtaki Baraza alipwe fidia, naye Meya apate fungu lake.

SEGERA FESTUS'S SOFT COPY HUB: 0720121995

(xxv) Meya na madiwani wanazorotesha uongozi kwa kutumia mbinu hasi za utawala kama vile propaganda, badala ya kuyashughulikia matatizo.

5. (a) (i) Haya ni maneno ya Meya.
(ii) Anamwambia Bili.
(iii) Wamo afisini mwa Meya.
(iv) Meya anaelezea sababu za kuwapeleka wanawe ng'ambo kusomea huko.
(4 x 1 = 4)

**Tanbihi**

Dondoo limetolewa uk.25. Nakala nyingine zinaweza kutofautiana ki-ukurasa.

(b) Kinaya, Meya anaikosoa elimu ambayo anastahili kuiboresha. (alama 2)

**au**

Kejeli/dhihaka/ stihizai. Meya kuidunisha elimu. Meya anajidhalilisha kwa kudunisha
elimu ambayo anastahili kuiboresha mwenyewe. (alama 2)

(c) **Kinaya**

(i) Kauli ya Meya inadokeza kuwa yeye ni mzazi mwenye busara (kuona mbali) na hali anahiari kutumia pesa nyingi kuwasomeshea wanawe ng'ambo badala ya kuboresha elimu humu.;
(ii) Meya anawadanganya raia kwamba dawa zimeagizwa ilhali sivyo, hatutarajii haya kutoka kwa kiongozi.
(iii) Meya anadai Cheneo ni kisiwani cha hazina na hali watu wanakufa (yule mtoto) kwa kukosa huduma za afya.
(iv) Badala ya Meya na madiwani kuendeleza mpango wa kimaendeleo wa mji, Meya anadai kwamba wanathamini malengo ya kimilenia na hali kwa kweli hata haya hayashughulikiwi.
(v) Meya anamruhusu Bili kuiba fimbo ya Meya ambayo kwa kweli ndiyo kitambulisho cha umeya.
(vi) Meya anampeleka mkewe kujifungulia ng'ambo badala ya kuimarisha huduma za kiafya Cheneo.
(vii) Meya anataka mwanawe apate uraia ng'ambo na hali yeye ni kiongozi anayetarajiwa kupalilia uzalendo.
(viii) Meya anabadhiri mali ya umma kupitia '*entertainment vote*', huku akidai kuwa ni matunda ya jasho lake. Haya hayatarajiwi kwa kiongozi.
(ix) Meya anaidhinisha kuongeza mishahara ya madiwani ilhali Baraza lina nakisi ya fedha.
(x) Meya kulalamikia udogo wa mayai na hali watu hawana chakula.

SEGERA FESTUS'S SOFT COPY HUB: 0720121995

(xi) Meya analipagaza baraza deni badala ya kulisaidia kutumia fedha vyema.

(xii) Meya analalamikia kupunjwa kwa kuletewa viyai vidogo na hali yeye anawapa wafanyakazi mishahara duni.

(xiii) Watu wanamchagua Meya wakitarajia kuimarika kwa hali zao za maisha. Meya anaishia kuwatelekeza katika njaa na magonjwa .

(xiv) Meya anaidhinisha pendekezo la Diwani II la kuundwa kwa kamati za kuhudumu na hali anafahamu kwamba baraza halimudu gharama hii.

(xv) Ni kinaya kutarajia mama muuza ndizi kulipa kodi na hali Meya anawaruhusu walionacho kama vile madiwani na kutolipa.

(xvi) Meya, badala ya kudhibiti matumizi mabaya ya mali ya umma, anajigawia vipande vinane vya ardhi na kumgawia Bili pia.

(xvii) Ni kinaya kwa Meya kutomshughulisha Diwani III katika maamuzi yanayohusu matumizi ya fedha na hali ndiye mtaalamu katika masuala haya.

(xviii) Ni kinaya kwa Meya kumruhusu Diwani I ambaye anastahili kulihakikishia Baraza usalama kufanikisha wizi wa fimbo ya Meya.

(xix) Meya anaidhinisha Baraza kutoa sadaka ya shilingi laki moja kila mwezi na hali anajua lina nakisi ya fedha.

(xx) Badala ya Meya kushughulikia matatizo ya raia, anaeneza propaganda kupitia Diwani I kuhusu kujitolea kwa Baraza kutetea demokrasia.

(7 x 2= 14)

**Au**

Mtahiniwa anaweza kuibua hoja zifuatazo kuhusiana na kejeli.

**Kejeli**

(i) Anwani ya tamthilia inafumbata kejeli kwa kumwita Meya mstahiki na hali hata anaidhinisha wizi wa fimbo yake.

(ii) Meya anajidhalilisha kwa kulalamikia mambo madogomadogo kama vile mayai.

(iii) Uongozi wa Meya unadhihakiwa kwa kushindwa hata kuiendesha zahanati. Zahanati haina hata dawa za kimsingi.

(iv) Meya anaikejeli elimu ya humu nchini kwa kusema ni duni mno; kwa njia hii anajidhalilisha pia kwani yeye anastahili kuchangia kuiboresha .

(v) Meya anajidhalilisha mwenyewe kwa kumwachia Bili kuliendesha Baraza na hali Bili si mtaalamu katika masuala ya uongozi.

(vi) Meya anaudunisha uongozi wake kwa kuidhinisha nyongeza ya mishahara ya madiwani huku akifahamu kwamba hazina ya Baraza haimudu kugharamia nyongeza hii.

(vii) Mwandishi anamkejeli Meya kwa kumfanya kushindwa kung'amua udanganyifu wa Bili.

(viii) Mwandishi anamkejeli Meya kwa kumfanya kutumia pesa za msaada kuagizia

SEGERA FESTUS'S SOFT COPY HUB: 0720121995

mvinyo kutoka ng'ambo na kuishia kurudisha pesa hizo hizo huko ng'ambo.

(ix) Meya anadai kwamba kungekuwa na Phd ya uongozi angekuwa nayo na hali anaendeleza mbinu hasi za uongozi kama vile propaganda.

(x) Meya anasawiriwa kama mwenye mawazo finyu, anayeshindwa kuona umuhimu wa mpango wa kimaendeleo wa Cheneo.

(xi) Meya anadhihaki uongozi wake kwa kuidhinisha malipo kwa kazi ambayo haijatekelezwa. Anaidhinisha kulipwa kwa Bili.

(xii) Meya anajidhalilisha kwa kulipagaza Baraza deni. Anakubali mshawasha wa Bili kwamba amwambie mwanakandarasi alishtaki Baraza n.k.

(xiii) Meya amajidhalilisha kwa kudai kuwa ni mzazi mwenye kuona mbali na hali Hata anashidwa kung'amua umuhimu wa usafi. Pia anahadaiwa na Bili kwa urahisi.

(7 x 2= 14)

**Tanbihi**

(i) Hoja zinazohusu kinaya zinaweza pia kujadiliwa kama kejeli au stihizai, mradi mtahiniwa amezifafanua zikaeleweka kuwa ni Kejeli.

(ii) Mifano yote, ihusiane na Meya hata kama inawarejelea wahusika wengine.

(iii) Baadhi ya watahiniwa, ambao si makini, huenda wakachukulia kuwa tamathali ya usemi iliyotumiwa ni **nahau** au **msemo** (anayeona mbali). Hawa washughulikiwe kulingana na jinsi wanvyojieleza na kutoa mifano. Hata hivyo, mifano ya semi wanayotoa lazima, ihusiane moja kwa moja na Meya.

**Ushairi**

6. (a) Mzungumzaji (nafsineni) asingiziwa ugumba hasa kwa kutoshiriki mapenzi nje ya ndoa.

(1 x 2 = 2 )

(b) Mambo ambayo anapinga ni:

(i) Kuiga rika; hususa kushiriki ulevi pamoja na kufukuza wasichana

(ii) Mzungumzaji kupakwa tope (kuaibishwa) kwa kuwa yeye ni gumba

(iii) Wamsemao kudai kuwa anatamani kuwa kama wao

(iv) Eti kuwa ugumba na ukapera ni kosa

(v) Kuharibu maisha kwa ujana

(vi) Kusingiziwa atapenda (atatamani) hali za wamsemao

(vii) Watu kueneza uvumi kuwa yeye ni gumba (5 x 1 = 5 )

(c) Umuhimu wa viishio

(i) Viishio hivi ni vifupi na hivyo vinatoa ujumbe kwa namna iliyo madhubuti

(ii) Viishio hivi vinaunga ujumbe wa kila ubeti/vinasisitiza ujumbe; wa shairi

(iii) Viishio vinachimuza/kuonyesha/kubainisha dhamira au mwelekeo wa mshairi kuhusu hali ya vijana kujiingiza katika mahusiano yasiyofaa.

(1 x 2 = 2)

(d) Mtindo ufuatao unaweza kukubalika:

Ni jambo gani ambalo linamkasirisha Mungu ambalo halikubaliki kanisani? Je, ni mtu kuwa kahaba na mwenye vioja ama mtu aliyezaliwa akiwa tasa? Kuwa gumba au kapera si kosa na wala haliwezi kuwa kosa. Kwa kweli mimi sina makosa. (4 x 1= 4)

(e) (i) Kila ubeti una mistari minne.

(ii) Mistari mitatu ya kwanza ina viapande vitatu ilhali wa nne una kipande kimoja.

(iii) Vina katika kila kipande vinabadilika kutoka ubeti mmoja hadi mwingine.

(iv) Kiishio kimefupishwa.

(v) Kila mstari una mizani 20 isipokuwa kiishio chenye mizani 8.

(vi) Shairi lina beti 5.

(4 x 1 = 4)

(f) (i) Mbio za wasichana - uasherati/uzinzi/uzinifu

(ii) Haupandiki mgomba - hana uwezo wa kujamiiana.

**7.** (a) (i) Shairi hili ni wasia kwa vijana; unaowaonya dhidi ya kushiriki mapenzi.

(ii) Linashauri kuwa wanaovutia machoni wanaugua na hivyo wanaweza kuwaambukiza maradhi yasiyotibika.

(iii) Zinaa hii haichagui wala kupendelea yeyote. Hata wenye nguvu au warembo wamesalimu amri (ubeti 4).

(iv) Vijana wajikaze kuhakiksiha kuwa hawaingii kwenye mtego wa kushiriki mapenzi.

(v) Wapo watakaowasema wenye kujitunza lakini hilo lisiwafanye kutetereka.

(4 x 1= 4)

(b) (i) Tabdila - Kubadili miendelezo ya maneno pasi na kubadili idadi ya mizani. Neno ‘nisikia’ lingekuwa ‘nisikie’.
Limetumiwa hivi ili kukidhi mahitaji ya vina.

(ii) Inkisari - kufupisha maneno. Inkisari imetumiwa kuleta ulinganifu wa mizani. Maneno yaliyofupishwa nikama vile:

(a) ‘Sikuwambia’ badala ya ‘Sikuwaambia’

(b) ‘Jepusheni’ badala ya ‘Jiepusheni”

SEGERA FESTUS’S SOFT COPY HUB: 0720121995

(c) ‘ngawa’ badala ya ‘ingawa’
(d) ‘waone’ badala ya ‘uwaone’ (2 x 1 = 2)
(e) ‘mkamba’ badala ya ‘mkaamba’
(f) ‘ngia’ badala ya ‘ingia’
(g) ‘walopapia’ badala ya ‘waliopapia’
(h) ‘watalokwamba’ badala ya ‘watakalokwamba’

(iii) Miundo ngeu ya kisintaksia / kuboronga sarufi. Mpangilio wa maneno katika tungo haufuati utaratibu wa kisarufi wa lugha ya Kiswahili. Baadhi ya matumizi
ya mbinu hii ni:
(a) ‘yaugua nisikia’ badala ya ‘nisikie yaugua’
(b) ‘si mlango nyumba nzuri’ badala ya ‘nyumba nzuri si mlango’
(c) ‘makaa kujipalia’ badala ya ‘kujipalia makaa’
‘madhara kukadiria’ badala ya ‘kukadiria madhara’
‘mapoda kumichia’ badala ya ‘kumichia mapoda’

(iv) Mazida - ‘vyang’aria’ badala ya ‘vyang’ara’
(v) Utohozi - Sitoria - history
Mazida na utohozi zimetumiwa kuleta urari wa vina
Mbinu (4 x 2 = 8)
Kutaja - alama 1
Kufafanua, au mfano - alama 1

(c) Pande mbili ambazo mshairi anasema nazo ni:
(i) Vijana (ubeti 1 - 8)
(ii) Mungu (ubeti 9)
(2 x 1 = 2)

(d) Umuhimu wa maswali ya balagha.
(i) Maswali ya balagha ambayo yanalenga msomaji wa kazi ya fasihi hunuiwa kumfanya kulitafakari jambo hivyo kujifunza kwalo.
(ii) Humfanya msonaji kulidadisi jambo linaloibuliwa. Katika ubeti wa sita msomaji atavuta fikra kuhusu ‘faida’ ya kuingia kwenye anasa ya kumuua. Kwa kulidadisi hili ataona kuwa hamna faida na hivyo kujirudi.
(iii) Hutumiwa kusuta watu au kukashifu jambo. Ubeti wa 5 unawakashifu waliopapia anasa na kuwatahadharisha wasomaji kwa kuonyesha kuwa hatima ya anasa ni kifo.
(iv) Hutumiwa kusisitiza wazo au kumfanya msomaji kushawishika na mtazamo wa msanii. Kwa mfano, katika ubeti wa 6, mshairi anamshawishi msomaji kwamba hakuna faida ya kuingilia anasa.

SEGERA FESTUS’S SOFT COPY HUB: 0720121995

(v) Hutumiwa kuzindua. Ubeti wa 5 unamzindua msomayi kuona kuwa hata wenye nguvu huangamizwa na zinaa

(3 x 1 = 3)

(e) Toni ya huzuni/ kusikitika

(i) Anasikitikia madhara yatakayowapata wanaoingilia, zinaa kwa kauli kama vile 'wawapi leo madume, anasa walopapia'?(ubeti 5)

**Au**

(ii) Toni ya kunasihi au kushawishi. Anawasihi vijana kuepuka zinaa. Kwa mfano anawaambia, "kikiki ikaze kamba, u kijana vumilia". (ubeti 7)

(iii) Kukejeli/kudharau/stihizai/bezo.

(iv) Uchungu - anaonea uchungu tabia ya vyana.

Kutaja - alama 1

Kueleza na kutoa mfano - alama 2

(1 x 3 = 3)

**8.** (a) (i) Mandhari ni nyumbani mwa Mzee Babu.

(ii) Wanatekede wamekusanyika kwa Mzee Babu kujadili kuhusu mabadiliko ya hali ya anga.

(iii) Bi Cherehani na Bwana Pima ambao ndio washona kikaza wamo kikaoni.

(iv) Bwana Machupa amemwomba mzee Babu kuwafafanulia kitendawili cha hali hii ya anga

(v) Mzee Babu anawaambia wanakijiji wawaulize washona kikaza. (Cherehani na Pima)

(vi) Wanapoulizwa hawatoi jibu la kuridhisha, wanasema ndio mtindo na walifuata mtindo.

(4 x 1= 4)

**Tanbihi**

Dondoo limetolewa uk. 42

(b) Maneno kiini katika swali hili ni **wanavyofuata mitindo na kuacha chungu kinatokota bila kuivisha**

Watahiniwa wanaweza kulifasiri swali kwa namna zifuatazo:

(a) Watu/viongozi kutoshughulikia hali inayowakabili

(b) Viongozi kufuata mitindo ya uongozi ya viongozi watangulizi badala ya kuiboresha

(c) Watu kufumbia macho makosa ya viongozi

(d) Viongozi kusaliti nafasi yao kwa kuendeleza uovu na uharibifu badala ya kuukosoa, nk.

(e) Viongozi na raia kuendeleza vitendo na hali hasi kama vile tamaa na ubinafsi

(f) Raia kuwawekea vikwazo viongozi na kungojea waporomoke.

Hoja zifuatazo zinaweza kujitokeza.

(i) Kobe anachangiwa manyoya na ndege kupaa angani lakini wanapofika anakula wanavyopewa bila kuwagawia waliomkweza ila waliobahatika kupata makombo.
(ii) Mtajika anahujumu demokrasia kwa kupata kura kwa njia ya udanganyifu.
(iii) Mtajika hafanyi lolote kutatua shida za wanakijiji. Tunaambiwa mambo yakiwa mabaya hasemi lolote kwani ameshapata aliyotaka.
(iv) Viongozi wanawasaliti washona kikaza (wapiga kura) kwa kuwadharau, kuwapuuza na kutowathamini licha ya kwamba ndio waliowachagua.
(v) Wanakijiji (raia) wanajua Mtajika amevunja masharti ya kikaza (uongozi) lakini hawamkosoi, wananyamaza, wanayafungia macho makosa ya viongozi.
(vi) Mtajika anamruhusu mkewe kukishika kikaza (kuingilia uongozi) kinyume na kaida za jamii.
(vii) Bi Mtajika anavunja kanuni za uhusiano mwema hata katika sherehe. Hata anatamka kuwa hakuna kiongozi mwingine kushinda yeye.
(viii) Viongozi wanayaharibu mazingira badala ya kuyahifadhi. Tunaambiwa jibu la kitendawili cha mawingu bila maji limo katika kikaza.
(ix) Machupa ambaye ni msemaji wa wanakijiji si wa kutegemewa. Anafaidika kwa Mtajika. Tunaambiwa kwamba yeye huenda na (huunga) upande unaomfaidi. Tunaambiwa alijua namna ya kuishi.
(x) Viongozi wamewatelekeza raia kwenye njaa na magonjwa (uk 47).
(xi) Mtajika amewaaibisha wanakijiji kwa kutokilinda kikaza (uongozi). Bi Chirenga anasema kikaza kimepasuka.
(xii) Mtajika na wenzake wanaipora mali ya umma; wanaifukarisha jamii kwa ubinafsi wao. Tunaambiwa kama ni nguruwe walijua kuchagua (uk 47).
(xiii) Raia kutokuwa na uwajibikaji wa pamoja japo wote ni washiriki katika ushonaji wa kikaza (uteuzi wa viongozi). Wanawatarajia Bi Cherehani na Bwana Pima kuelezea kitendawili cha kutonyesha kwa mvua (uk 42).
(xiv) Raia kutowajibikia vitendo vyao. Wanashiriki katika ushonaji wa kikaza (uteuzi wa viongozi) bila kuwazia uzito wa tendo hili. Wanachagua viongozi ambao wanawaathiri wenyewe (uk 43- 44).
(xv) Viongozi wanakwezwa uongozini na raia kisha wanawatelekeza pindi tu wanapofika kileleni (istiara ya kobe - na ndege (uk. 44).
(xvi) Vikaragosi wanashirikiana na viongozi kuwadhulumu wanyonge. Kobe na vibarakala wake wananyakua kila kitu na kuwaachia wachache waliobahatika masalio (uk.44).
(xvii) Raia wanashiriki katika uharibifu wa mazingira na kusababisha kutotegemewa kwa hali ya anga. Mvua, ama inanyesha nyingi kupindukia, au hainyeshi kabisa

SEGERA FESTUS'S SOFT COPY HUB: 0720121995

(uk. 40). Machupa anawaambia wanakijiji kuwa jibu la kitendawili cha wawingu bila maji ni kikaza na raia ndio wenye kupima na kushona kikaza (uk. 46).

(xviii) Viongozi kuendeleza uongo na udanganyifu. Mtajika angeubadilisha ukweli kuwa uongo na uongo kuwa ukweli (uk 44).

(xix) Badala ya viongozi kushughulikia uhalisia wa mambo, wanaishi katika ulimwengu wa ndoto. Hata nchi inapokumbwa na changamoto, Bwana Mtajika anaota tu badala ya kukabiliana na changamoto zenyewe (uk. 44). Hata raia wanapoutaka ushauri wake, hasemi lolote; ashapata aliyopangia kupata (uk 44).

(xx) Raia wanaogopa, hivyo wanayafumbia kinywa matendo hasi ya viongozi. Tunaambiwa ni wachache wanaoweza kusema ukweli, hasa unaohusu viongozi (uk. 45). Bwana Mtajika anavunja kaida za kikaza (Kaida za uongozi) na hawamkosoi.

(xxi) Unafiki wa baadhi ya raia unaifanya Tekede kudorora kimaendeleo. Tunaambiwa kuwa Machupa hula kuwili. Anasikiliza wasemayo wanakijiji kumpelekea Mtajika na hapohapo anawaonyesha wanakijiji kuwa tatizo limo kwenye uongozi. Yeye anajitoa lawamani badala ya kushirikiana na raia kutatua tatizo la uharibifu wa mazingira (uk. 46).

(xxii) Viongozi wanawatelekeza raia waliowachagua katika njaa, umaskini na ugonjwa. (uk. 47).

(xxiii) Bwana Mtajika anashindwa kuulinda uongozi: anashindwa kulidhibiti taifa. Cherehani anasema kwamba kikaza kimepasuka.

(xxiv) Wizi wa mali ya umma unawafanya wafuasi wengine wa Mtajika kutotaka kuonekana hadharani isipokuwa Machupa ambaye anajua namna ya kuishi (uk 47). Hivyo viongozi hawadiriki kutatua matatizo ya raia.

(xxv) Raia wanawawekea viongozi vikwazo vinavyosababisha kuanguka kwao. Cherehani anapunguza kiwango cha kikaza maksudi; kikaza kinapasuka. (uk 48)

(8 x 2 = 16)

SEGERA FESTUS'S SOFT COPY HUB: 0720121995

**102/2**
**KISWAHILI**
**USAHIHISHO**
**KARATASI 3**
**FASIHI YA KISWAHILI**
**OKT/NOV 2014**
**SAA 2 ½**

1(a)

i. Kauli ya kwanza ni ya Amani kwa Imani
ii. Kauli ya pili ni ya Imani kwa Amani
iii. Wamo kibandani kwa Amani
iv. Anamwadithia Amani kuhusu kadhia iliyompata; mama yake kupigwa,kufa kwake na kuchomewa nyumba na kukashifu wanakijiji cha Baraka kwa kutofanya lolote kumtetea. 4x1=4

(b)

i. Kinaya/kweli kinzani-mtu kufurahia msiba kwa wengine.
ii. Tankuzi -msiba na arusi ni vinyume-kuonyesha uovu/ugumu wa moyo.
iii. Sitiari/jazanda-msiba-tatizo.
   -arusi-furaha.
   -mzigo wa mwenzio kanda la usufi-kudunisha matatizo ya wengine.
   -msiba kwa wengine kwake arusi-kufurahia matatizo kwa wengine.

iv) Methali- mzigo kwa wengine ni kanda la usufi. za kwanza 2x1=2

(c)

i) Raia wa Braka,badala ya kumponza imani wanaogopa hata kuonekana wakiongea naye,wanaendelea tu na shughuli zao.
ii) Viongozi wanawadhuluma hata wale hawana chochote. Nasaba Bora anawadhuiuma kina imani shamba iaona kujifaidi kwalo./shamba la Chichir Hamadi
iii) Nasaba Bora anamuua Chichiri Hamadi na kunyakua mail yake.
iv) Nasaba Bora anampaza Amani Uhuru huku akijua si mototo wa Amani. Hata anatarajia Amani kuendelea nakazi yake yauehtmgazi pamoja na ulezi huu.
v) Nasaba Bora anashtriki mapenzi na msichana mchanga-towela-bila kujali mustakabali wake,na uchungu anowapa wengine kama Ben Bella na Mashaka.
vi) Nasaba Bora anakitupa kitoto chake langoni pa Amani ili kujitoa lawamani bila kuwazia afya yacho.
vii) Nasaba Bora anamwachia mkewe upweke huku akitafuta raha kwa wasichana wadogo

SEGERA FESTUS'S SOFT COPY HUB: 0720121995

kama vile Lowela.

viii) Nasaba anampiga Amani kikatili kwa shutuma zisizo na ithibati na kumtupa; anachojaii ni kulipiza kisasi tu.

ix) Fao anamwendea kinyume mwanafunzi wake kwa kuhusiana naye kimapenzi bila kujali unyonge wake kama mwanafunzi. Anapomtunga mimba anondoka bila kujali hali ya mtoto na mama yake.

x) Michelle anakataa posa ya majununi hata baada ya Majununi kujikalifu kujenga jumba ili kutimiza masharti yake.

xi) Majisifu anamwibia Amani mswada na kujifaidi kwao, hajali yatayompata Amani.

xii) Majisifu, badala ya kuhudhulia madarasa, anaingia ulevi bila kujali maendeleo ya wanafunzi wake.

xiii) Wenzake Amani chuoni wanamsingizia uchochezi na kumfanya kufungwa na kukatiza masomo yake.

xiv) Nasaba Bora anawafungia Amani na Imani kwa madai kwamba amekiua kitoto japo kimekufa kwa kichomi

xv) Wauguzi hospitali wanakosa kukitibu kitoto, wanasema ni Sikukuu,hawafanyikazi, na kusababisha kifochacho,huku wakiendelea na shughuli zao.

xvi) Serikali inawatekeleza wazalendo,kama vile Mtuko Weye, hata anaposema ukweii kuwahusu viongozi.

xvii) Nasaba Bora anamtaliki mkewe kwashutma ambazo hajathibitisha, licha ya kwamba mkewe amekuwa mwaminifu kwake. Nasaba Bora anaendeleza uhusiano na Lowela.

xviii) Serikali inawatekeleza wachezaji kama Makweche katika umaskini na ugonjwa hata baada ya kuiletea nchi sifa. Makweche anaishia kukatwa mguu.

xix) Askari wanampiga mamke Imani machoni mwake bila kujali dhiki ya kisaikolojia wanayomsababishia. Baadaye mama imani anakufa kwamaumivu haya.

xx) Oscar Kambona ,baada kuuawa kwa mamake anaondoka bila kuaga,anamwachia Imani ukiwa.

xxi) Wahudumu katika zahanati hawashughulikii DJ. DJ analazimika kuondoka hospitalini kutafuta matibabu kwingine.

xxii) Serikali badala ya kufadhilimu eiimu ya maskini,inatumia pesa kudhamini elimu ya wanaojiweza kama vile Fao. fao anapelekwa kusomea ngambo.

xxiii) Nasaba Bora anashurtisha raia kuchangia elimu ya mwanawe Madhubuti hajali hafi yao duni kiuchumi. Madhubuti anakwenda kusomea Urusi.

xxiv) Majisifu anawadharau wanawe wenye mahitaji maalum. Anawachia mkewe malezi bila kujali dhiki anazomsababishia. Hawapeleki wanawe shuleni au kwa uangalizi maalum.

xxv) Nasaba Bora badala ya kuwahudumia raia katika Afisi ya Wizara ya Ardhi anaficha faili na kuwalazimisha kutoa hongo ili kuwahudumia.

xxvi) Nasaba Bora hajali afya ya majibwa yake, hayachanji/Zuhura kutohurumia majibwa yake na kusema ni majibwa tu DJ anapomwuliza.

SEGERA FESTUS'S SOFT COPY HUB: 0720121995

xxvii) Nasaba Bora anawafuta wafanyakazi wake kiholeia,hata kwa kunadhlfisha maskani yake, hajali watapata wapi riziki,

xxviii) Mama anayejifungua anawachwa pale na Nasaba Bora. Zuhura anajaribu Nasaba Bora ambebe lakini anakataa.

xxix) DJ kuumwa na jlbwa ,Mtemi anaendelea kusoma Biblia hata Zuhura anapomwambia hajali.

xxx) Wazungu wananyakua mashamba na kuwaacha waafrika bila mashamba.

xxxi) Wazungu kuwakataza waafrika kukuza mimea na kufuga mifugo.

xxxii) Mashaka kuwabeza watoto walemavu wa Mwalimu Majisifu na msiba kwa wazazi wao.

xxxiii) Majisifu anaposhidwa kutoa mhadhara wanafunzi wanamcheka na kumkejeli.

xxxiv) Yusufu anasingiziwa mauaji ya babake na anafungwa maisha.

xxxv) Mtemi Nasaba Bora kumficha Lowela ilhali wazazi wake wanahangaika kumtafuta

xxxvi) Mtemi / viongozi kuvuja pesa za kujengea hisipitali na badala wanajenga zahanati.

xxxvii) Uasi wa Madhubuti ni msiba kwa Nasabora bali ni arusi kwake Madhubuti.

7x2=14

2 (a)

i) Ni maneno ya Diwani 1.

ii) Ana mwambia Meya .Diwani ii, na Diwani iii/madiwani

iii) Wamo ofisini mwa Meya

iv) Meya amewaita ili waweze kutafuta mbinu za kuwadhibti watu ambao anadai wamechochewa na baadhi ya madiwa ni kulalamikia hali ya baraza kushindwa kujimudu./kukabiliana na mgomo 4x1=4

(b) Matumizi ya vitisho/kunyanyasa,diwani 1 anasema watakaogoma watafutwa 1x2=2 )

(c)

i. Hila/udanganyifu/unafiki/uongo-Meya anahidi dawa ambazo hazimo, ili watu watulie/virungu kupunguzwa wakati wa migomo kwa sababu uchaguzi unakaribia.

ii. Uteuzi wa washauri ambao ni Baraka wa meya. Diwani wa kwanza anasema kwamba jukumu lao ni kulinda baraza la Mstahiki Meya ,wanalipwa sababu hii

iii. Propaganda-Kutangazwa kujitolea kwa Baraza kuleta demokrasia na halt sivyo.
   - Mashindano fcupeperushwa kupitia vyombo vya habariili kuibua hisia za kizalendo.

iv. Uundaji kamati za kuhudumu (za madiwani}- Madiwani wenye ushawishi mkubwa wameteuliwa ili kusiwe na upinzani.Meya hajali pesa zitakazo tumiwa kuendesha kamati hizi.

v. Hongo/vishawishi-meya anahidhinisha nyongeza ya mishahara ya madiwani na kutotozwa kodi ili wamuunge mkono/kubatilishwa haki/unyakuzi wa ardhi/kuajiri watu

wa ukoo/mhazili/mapendeleo ili watu wamuunge mkono ilhali wafanyakazi hawaongezewi mshahara na wanatozwa kodi.

vi. Meya anakabiilana na migomo ya wafanya kazi kikatili (kupigwa)-Askari wanawatanya wafanyakazi waliogoma /kuuawa.

vii. Kuunda sheria ambayo inampa Meya mamlaka yanayomfanya kuongoza kwa mbavu-Mayors Act inampa mamlaka ya kumnyamazisha yeyote anayempinga.

viii. Kuwatenga washauri/viongozi wanaompinga meya. Maamuzi yanayohusiana na pesa yanatolewa naDiwani 1 na diwani II huku wamemtenga Diwani 111.

ix. Kujilinganisha na mataifa dhaifu kiuchumi iii kuonekana na raia kwamba wameendelea, akisema kwamba Cheneo ni Kisiwa chenya amani, Siki akimwonya dhidi ya kujiiinganisha na chumi dhaifu.

x. Kufukarisha wanyonge /bei ya vitu iii awatawale.

xi. Misaada -anatumia misaada hiyokuwastarehesha wageni badala ya kuendeleza nchi.

xii. Meya anatumia dini/mhubiri anapokea pesa iii kutuliza watu wasimpinge meya.

xiii. Mapuuza -viongozi (meya) wartapuuza wafanyakazina malalamishi yao na kusema ni wahitaji watarudikazini /sema watawaajiri vijana. (Za kwanza 7x2=14)

3

i) Wagonjwa wanaambiwa wangoje dawa ziiizoagozwa 'ambazo kwa kweii hazijaagizwa baadhi waishia kufa-mtoto wa Kerekecha.

ii) Kutoshughuiikiwa kwa mishahara ya wafanyakazi na kutofooresha hali yao ya maisha na utenda kazi kuna sababisha mgomo wa wafanyakazi

iii) Malimbikizi ya mishahara ya wafanyakazi kuna wafanya wakate tama, baadhi wao kama Waridi anajiuzuru, wengine wanagoma.

iv) Kutoboreshwa kwa maisha ya wafanyakazi kunawafanya waishi maisha yasiyo na hadhi. Wanakula makombo.

v) Wafanyakazi wanakosa vifaa vya kufanyia kazi. Mji umeenea uchafu/glavu.

vi) Wafanyakazi wanaposita kuzoa kuzoa taka mji uarundikana uchafu. Uvundo unaenea hadi afisini mwa meya.

vii) Kurundikana kwa uchafu na tishio la mkurupuko wa magonjwa unawafanya wageni kutozuru Cheneo. Meya anaaibika.

viii) Meya anapuuza ushauri wa Diwani 111 kuhusu matumizi ya fedha na kusabaishia Baraza nakisi ya pesa. Siki anamwendea Meya ili kumshauri na meya anakataa.

ix) Meya anakosa kuona udanganyifu wa Bili.anaishia kusababisha kuibwa fimbo yake y mwenyewe ambayo ni kiwakilishi cha umeya.

x) Raia wanapuuza umuhimu wa kuwachagua viongozi waadilifu. Wanawachagua viongozi dhalimu na kurithisha uongozi mbaya kwa kuchagua wabaya wakijua ni wabaya.

xi) Wanataaluma wanakataa kuingia kwenye siasa {mf.Siki), nchi inakosa huduma yao,uongozi mbaya unaendelezwa zaidi.

xii) Meya anapinga mpango wa maendeleo wa miaka kumi wa mji, akidai wao wanadhamini

malengo ya kimilenia.Cheneo inashindwa kuzua mipango ya kuzalisha pesa za kuongeza mishahara ya wafanyakazi.

xiii) Meya anakosa kudhibiti tama yake, anamruhusu Bili kumshawishi kulipagaza Baraza deni kupitia kesi ya mwanakandarasi. Meya anafaidi huku uchumi ukidorora.

xiv) Meya anashindwa kuurekebisha uongozi wake licha ya ushauri wa Siki na Diwani 111. Anudhoofisha uongozi wake na- kuishia kongoiewa uongozini.

xv) Meya anashauriwa na Diwani 1 na Diwani 11 kuundakamati nyingi, hawazii umuhimu wa kamati hizo. Anaishia kuifilisha hazina ya baraza.

xvi) Kutodhibiti mgomo wa wafanyakazi kwa kushughulikia malalamishi yao kunasababisha kutokusanywa kwa kodi, Baraza inapoteza fedha.

xvii) Baraza linashindwa kudhiti usalama mjini.Askari wameutwaa mji. Wanawafukuza wafanyakazi,wanawafanya watu kukaa tu nyumbani kutazama matukio yanayoendelea(mf Diwani 111)

xviii) Meya anapuuza umuhimu wa madiwani kulipa kodi na kusababisha kuzorota kwa pato la Baraza.

xix) Meya badala ya kuzalisha pesa kulipia mishahara anategemea kuzipata kutoka kwa wafadhili/washirika wao wa kimaendeleo. Hawazi kuwa huu ni mzigo unaorithishwa vizazi vya kesho. Anapalilia hali ya utegemezi.

xx) Hali ya baadhi ya wanyonge kujiwazia wao wenyewe inafanya hali ya jamii ya wanyonge kutobadilika. Dida anasema hajali haii ya meya kuwapeleka wati wake mbali na uvundowa mji mradi meya waendelee kuwapo naye aendelee na kazi yake duni ya kunadhifisha nyumba zao.

xxi) Meya anapuuza umuhimu wa kutumia pesa za umma vyema. Anabadhiri pesa kwa kumpeleka Bill kujistarehesha na kumpeleka mkewe kuzalia ngambo.

xxii) Meya anaendeleza hali duni ya elimu 'badala ya kuiboresha, anawapeleka wanawe kusomea ngambo.

xxiii) Meya anapuuza athari za mgomo wa wafanyakazi/anapuuza umuhimu wa wafanyakazi wa kima cha chini. Anamwambia Diwani lll.

xxiv) Meya anakataa kushughulikia changamoto za feo anasema kesho na mtondogoo hatakuwepo, hivyo hatna haja kujidhikt.

xxv) Badala ya meya kuhifadhi hazina ya Baraza, anafilisi zaidi kwa kumpa mhubiri sadaka ya elfu mia moja kila mwezi/dini.

xxvi) Meya anaongozwa na mtazamo finyu kulifilisi Baraza kwa kuagiza mvinyo wa kuwastarehesha wageni kwa kutoka ng'ambo.Anatumia pesa hizo hizowanazoteta kwa maraifaa ya hao hao wagmi /msaada.

xxvii) Meya anapuuza wajibu wa kuilinda ardhi ya Cheneojanajigawia ardht na kugawia Bill.

xxviii) Waridi kuwacha kazi kwa sababu ya ukosefu wa dawa. Vifo vya watoto zahanatini,uchafu

Tanbihi; Mtahiniwa aonyeshe pande zote mbili (ZOZOTE 10 X 2=20)

*SEGERA FESTUS'S SOFT COPY HUB: 0720121995*

4 (a)

i. Maneno ya Babu/Babu Maende
ii. Anamwambia mjukuu wake /msimulizi
iii. Wamo mtaa wa madongo/ wamo Kochokocho sehemu iitwayo Madongo
iv. Babu Ameona hafi duni/majengo duni yaliyosongamana, ndipo akasema baya/amewaona wanawake wanaokaanga samaki na kuwauzia wapiti njia katika, kitongoji biki duni, ndipo akasema haya. (4x1=4)

IIa

i. Anadhihirisha umuhimu wa raia kuendeleza elimu sehemu za mashambani badala ya kujudhiki kwa maisha duni mjini yanayopaliiia umaskini zaidi(uk.78)
ii. Anaonyesha hali kukatisha tamaa mjini.
iii. Anaendeleza maudhui ya usaliti. Anasema kwamba aidha ni uburu wa Sakata utaleta manufaa kwa wote, ila sivyo.
iv. Anakashifu ubaguzi kwa misingi ya utabaka/anakashifu utabaka. Anasema Sakata ina makabila mawili tu; maskini na tajiri.
v. Ni kieielezo cha wazalendo wanaopingaukabila. Kila mara aliwazungumzia wanawe kuhusu ukabila Sakata.
vi. Anadhihirisha na kupinga ufisadi Sakata.
vii. Anamjuza msimulizi akiwa mchanga kuhusu hafi hailsi katika jamil yake. msimufizi anamsikta babu akftaja manene kam vile uhuru, ukabila, bongo, ufisadi/anamsimulia haditbi.
viii. Anaendeleza mshikamano wa kijamii kwa kumkubalia mwanawe kuoa mke asiyetoka kwenye jami yake.
ix. Ni kielelezo cha mwanajamii mwenye bidii. Hapendi kuiacha mifugo yake kuja mjini, anakuja kwa shinikizo la mwanawe.

x. Anaonyesha uktkaji wa haki za kibinadamu. Umati una mpiga na kummua kwa tuhuma kuwa nia mwizi wa watoto.

xi. Kupitia kwake tunasawiriwa uozo katika jamii ya Sakata. Wizi wa watoto unaendelezwa.
xii. Anaonyesha madhara/hatima ya ubaguzi wa rangi. Anauawa kwa tuhuma kwamba ameiba motto kwa vile mtoto ana rangi tofauti na yake.
xiii. Kupitia kwake tunaona ukakamavu wa msimulizi-anamuuma mama aliyempiga Babu kwa kumtetea.
xiv. Anaonyesha umuhimu wa kutoa shukrani unapotendewa wema/maadili.
xv. Ametumiwa kuonyesha sifa za watu wengine kama za baba ya msimulizi k.m aliye na msimsmo thabiti. (zozote 4x2=8}

SEGERA FESTUS'S SOFT COPY HUB: 0720121995

(b) **i)** Kinaya /ukweli kinzani-ni -kinaya kwamba mchuuzi anamsihi msimulizi/Christine awakumbuke watoto na kuwaonea huruma na hafi Christine amekwisha kuavya mimba. (Kutaja -1   maeiezo -1} (1x2=2)

**AU** Kejeli/stihizai/dhihaka - mchuuzi anamdhihaki Christine kwa kumuomba awaonee watoto huruma na hali Christine ameavya mimba.

**II**

i. Ni kinaya kwamba wavuvi wanasagika kuvua samaki na faida inamwendea Peter.
ii. Ni kinaya kwamba Diogracias anawadharau kina Christine na hali ni Waafrika wenzake. *Anawazungumzia kiganda ili kuwadharararisha*
iii. Christine anadai kwamba ameokoka na hali anahusiana kimapenzi na Peter.
iv. Dorothy ambaye anasema ameokoka amwambii Chrstine moja kwa moja akome kuhusiana na Peter kimapenzi.
v. Ni kinaya kwamba Peter analalamikia hali duni Afrika na hali yeye anatoka kwenye tabaka duni huko kwao.
vi. Muuguzi Margret  na  Mariam,badala ya kumkataza Christine kuavya mimba wanamwacha tu aavye.
vii. Mchuuzi anamtaka Christine kununulia watoto peremende hali Christine ameavya mtoto wake. Hii ni njia ya kukejeli ukatili wa Christine.
viii. Peter, badala ya kuhuzunika kwa tendo la uavya mimba, anatabasamutu, na baadaye kumuuliza Christine iwapo anataka pesa.
ix. Licha ya Christine kuonywa na Diogracias anaendelea urafiki na Peter/alizijua tabia za Peter.
x. Ni kinaya kuwa Zac anajidai kuwa rafiki ya Christine ilhali hamwonyi kuhusu tabia hasi za Peter za ukware. (za kwanza 3x2=6}

5

i. Jamila hajaridhika. Duni analewa kupindukia hata lakabu yake-Duni inahalalishwa na ulevi huu.
ii. Hajaridhika kwa kuaibishwa na Duni anaporudi kijijini akiimba na kuwaghasi wakazi wa mtaa wa Sebleni.
iii. Ukaidi wa dharau ya Duni hairidhishi. Anakanywa na wanakijiji dhidi ya 'taarabu liakini anakataa.
iv. Wanasebebleni wamemtoa Duni maanani, wanamwona kuwa hana thamani mbele ya madebe ya taka. Hili haliwezi kuridhisha.
v. Jamila anatiwa wasiwasi na tabia ya Duni pamoja na umri wake mbichi anamsubiri Duni usiku kwenye roshani.
vi. Duni anamliza Jamila. Jamila hata anatamani ingekuwa mara ya mwisho kusikia wimbo

SEGERA FESTUS'S SOFT COPY HUB: 0720121995

wa Duni. Duni hajuti matendo yake mabaya kwa mke wake.

vii. Duni anampiga Jamila na hata kumpa majeraha makovu ya mwili

viii. Duni anamtusi na kumsimbulia (simango) Jamila.

ix. Jamila hajaridhika kwani ana mgogoro na nafsi. Anawaza ikiwa aufuate ushauri wa wanaomnasihi kutoka kwenye ndoa yenye utesi au abaki. Anamua kutousaliti moyo wake/Salim/Shangazi wanamsihi aondoke.

x. Hisia/matukio ya Duni hayawezi kutabirika. Jamila anapojaribu kumsaidia anamwambia amwache, hahitaji msaada; inabidi Jamila akubalikuwa Duni hahitaji msaada; anaweza kila kitu.

xi. Duni anamwangaisha Jamila kwa kumtaka Jamila kuleta chakula haraka japo kwa kweli Duni haki chakula hicho.

xii. Duni anamuumbua Jamila.tunaambiwa Jamila hana lile busu/urembo wa zamani, anaonekana mwenye simanzi hata akiwa usingizini

xiii. Jamila ana dhiki ya kisaikolojia. Usingizi wake ni wa machovu.

xiv. Jamila anishi kwa hofu ya kuchelea kuvunjika kwa ndoa yake na Duni. Anatumainia kuwa siku moja Duni atabadilika.

xv. Duni anarudi nyumbani usiku mkuu saa saba usiku /kuchelewa.

xvi. Duni anawatusi wakaziwa mtaa wake, hivyo tabia hii haiwezi kumridhisha Jamila.

xvii. Duni anamwaibisha Jamila hata kwa majirani, majirani wanasikia matusi anayomwaiwa na mumewe.

xviii. Jamila analazimika kujiweka bashasha pale Duni anaporejea akiwa mlevi ili kumridhia mumewe.

xix. Duni analala akiwa amevalia nguo atizoshindia ulevini/harufu ya pombe/uchafu.

xx. Maneno ya Duni ya kinyume yanamsumbua Jamila. Anamwambia awaambie watu ameridhika na hali hajaridhika. Hata Duni mwenywe anasema kwamba penzi penzi lina mmiujiza,kuonyesha kwamba yeye ana udhaifu mkubwa na Jamila ana ufdhaifu kwa kuishi naye.

{u.k57) (zozote 10x2=20)

**6(a) shairi**

i. Shairi linazungumzia tatizo la upofu mf.ngakua na mato.

ii. Kwamba mtu anayepatwa na tatizo la upofu huwa hawezi kufanya mambo ambayo zamani alimudu bila tatizo.

**AU** Nafsineni inasikitikia hali yake ya kutomudu kujifanyia mambo kwa sababu ya upofu.

(b)

i. **inkisari** -imetumika ili kudumisha ulinganifu wa mizani.

SEGERA FESTUS'S SOFT COPY HUB: 0720121995

ii. Mifano -ngaliandaa-ningaliandaa -ngalifanya-ningalifanya, ngatia -ningalitia

iii. **Tabdila**-imetumiwa ili kuleta urari wa vina. Mifano-mduwaa-mduara -apikae-apikaye

**iv. Tabdila**

-vinavyong'aa-kuipa utungo mabadhi ya kishairi

v. Kuboronga /kufinyanga sarufi

-ubeti2-maksudi yangu ngaliandaa-kutosheieza urari wa vvna.

(c)

Ningetumia miti ifiyopinda na yenye umbo mzuri/kutengenezea kijiti kwenye tundu la wimbombo/kupekecbea moto kwa ufundi mkuu kiwambono/ningekuwa fundi stadi katika upekechaji wa moto.

**Tanibhi -wimbombo**-kipande cha mti kilichotobolewa tundu, na kinachotumiwa kupekechea moto. **-ulindi**-ni kijiti kinachopekechwa kwenye wimbombo ili kutoa moto.

(d) Toni ya huzuni /toni ya kuomboleza/ya rnasikitiko

Mshairi anahuzunishwa na analalamikia hali yake ya upofu isiyomruhusu kujifanyia Mambo mengi

(e)

i Urudiji wa sauti k.m ubeti wa 1 - Mstari wa mwisho kila ubeti

ii. Urudiaji wa silabi ra ra ra/a,a,a,e/ngu ,ngu,ngu(vina}n.k

iii. Urudiaji wa maneno k.m ulo-ubeti wa 3, mato ubeti wa 1,9

iv. Usambamba/urudiaji wa vishazi/urudiaji wa miundo sawa ya mistari k.m ngalisana kito, cha kuchezea, ngalifinyanga chungu, cha mduwaa. Kutaja- alama 1' Mfano – alama 1 za kwanza 3x2=6

f. Nafsineni ni kipofu/ mtu asiyeona.ubett 1 anasema, ngakua na mato' ubeti wa 9 anasema, mato ndo malenga kanikimbia" (Kutaja-l, Mfano-l, jumla-l}

**7 Shairi (a)**

i. Hodari wa kufanya kazi/wenye bidii/wakulima hodari/wenye bidii / kujitosheleza / hawatutii hadi wapate.

ii. Wenye kujiamini

iii. Waliopuuza/hawana makubwa (hawasikiki)

iv. Hawana tamaa

v. Wenye kupinga utaghai/wa kweli

vi. Wenye/ndoto haizimiki

vii. Hawahini / huwapa watu haki yao / waaminifu

viii. Wazalendo

*SEGERA FESTUS'S SOFT COPY HUB: 0720121995*

ix. Wanaohangaika/wanaoteseka kupata/wanaosumbuka (za kwanza 5x1=5)

(b)

i. **Tashbihi**- kama watanga na ropini- kuonyesha jinsi walivyojitolea (bidii)
ii. **Tashisi/uhaishaji**- Tamaa za moyo kutii, kupigana na ulaghai-hapa tama za moyo na ulaghai vimpewa uwezo wa kutenda -
iii. **Nahau/msemo** -ndoto haizimti.Hawapotezi tumaini, kunyesha hali ya kutokata tamaa la haramu watu hawafi-kuonyesha hawafaidiki kwa wasichokifanyia kazi.
iv. **Hisi mseto**- ndoto haizimiki na jasho hawali hapa tendo au jambo linalohusiana na kuona (haizimiki) linahusishwa na Jambo au hisl ya kuonja/muonjo(kula-jasho hawali)
v. **Taswira**-kutwa kite na hiki kama watanga na njia -kuonyesha watu wanaoshughulika kufanya kazi kuiendeleza nchi
vi. **Sitiari/jazanda**- ndoto haizimiki-hawapotezi tumaini
vii. **Taashira**-watokwa jasho vijijini-bidii
viii. **Kinaya**-japo wasikia hawakosi kujiamini-kuonyesha kutokata tama. Kutaja-1, Umuhimu-1 t[za kwanza 3x2=6)

(c)

i. Mazida-vinyuani badala ya viywani ili kutosheleza mahitaji ya idadi ya mizani.
ii. Kufinyanga sarufi / kuboronga lugha/ miuondo ngeu/ukiushi wa kisintaksia/ ukiushi wa kimiundo mf.
    - tamaa za moyo kutii badala ya kutii tama za moyo
    - la haramu jasho hawali badala ya -hawali jasho la haramu
    - ya kesho kuwa hati njema badala ya hali kesho kuwa njeraa imetumiwa kupata urari wa Vina
iii. Udondoshaji wa maneno (kuacha neno) kama
    - pato ambalo la halali badala ya pato ambalo ni halali
    - wiki baada wiki-wiki baada ya wikiumetumiwa ili kutosheieza idadi ya mizani/kupwnguza idadi ya mizani
iv. utohozi -mf, Wiki (kutaja -1 mfano -1 ,za kwanza3x2=6)

(d.) Tathilitha/wimbo/utatu- mishororo mitatu katika kila ubeti
Ukara-vtna vya kati/ndani vrnafanana katika shairi zima, vya nje vtnatofautiana
Kikwamba-kiia ubeti unaanza kwa kirai/maneno mfano; watafuta riziki (3x1=3)

**8. Aina ya ngano**

a) I Kisasili/kisasili cha usuli.lnazungumzia asili ya kifo (1x2=2)

**I umuhimu**

1. Hutumiwa kuelezea chanio cha mazoea ya kidini/kijamii. K.m asili ya dhehebu Fulani, asili yakifo.
ii. Ni tungo zinazo hatatisha baadhi desturi na imani za kidini za jamii.
iii. Ni kitambulisho cha jamii. Kila jamii ina visasili vyake vina vyohusiana na imani zayo/kioo cha jamii.
iv. Hurithisha imani, desturi na historia ya jamii kwa kuvitamba kwa vizazi mbalimbali.
v. Ni nyenzo ya kuadilisha .Kila kisasili huwa na adili k.m kisasili bapo juu kinafunza haja ya kutandarukia mambo/onyo ya kuasilisha

vi. Kuimarisha utangamano wa jamii. Watu wanapokuja pamoja kutambiana hujihishi kuwa kundi moja, hivyo umoja kujengeka.
vii. Hutumiwa kupunguza athari za baadhi ya mambo ya kimaumbile au misiba inayompata binadamu. K.m kisasili kuhusu chanzo cha kifo hutumiwa kuwapunguzia wanajamii mwemeo wa huzuni.
viii. Huburudisha. Watu wanapotambiwa huburudika na kuliwaza.
ix. Hurithisha fani yenyewe ya utambaji kwa vizazi mbalimbali.
x. Hukuza ubunifu. Kadri mtu anavyotamba ndivyo anavyopailia kipawa cha kubuni mitindo ya kuisimulia hadithi.
xi. Hukuza hukakamavu wa kuzungumza hadharani. Kadiri mtu anavyotamba ndivyo anavyopalilia ujasiri wa kuzungumza hadharani.
xii. Ni njia ya kuthibiti matendo nasi ya wanajamii. Baadhi ya visasili huzungumzia maeneo matakatifu kama vile madhabahu na hata mibuyu. Watu huelekezwa kuheshimu mahali hapa.
xiii. Hutumiwa kupitisha muda. Watu hushiriki vikao vya utambaji wakingojea shughuli nyingine
xiv. Hukuza lugha k.m msamiati kama mulungu.
xv. Huelimisha jamii/funzo.
xvi. Huhifadhi utamaduni, desturi na imani za jamii mbalimbali. (zozote 5x2=10)

**(b)Fomyula ya kumalizia**

i. Huonyesha kumalizika kwa ngano, hivyo kufunga muktadha ulimwengu wa usimulizi/ulimwengu usio halisi.
ii. Hapa ndipo fanani hutangaza adili au funzo la usimuluzi wake.

iii. Baadhi huwapa wasikilizaji changamoto ya kuwa watambaji bora, hivyo kurithisha stadi bora za utambaji.
iv. Humpisha mtambaji anayefuata. Anaweza kuashirwa kwa kauli Fulani au kwa kupa changamoto.

*SEGERA FESTUS'S SOFT COPY HUB: 0720121995*

v. Huitoa hadhira kwenye ulimwengu wa ubunifu na kuwaingiza kwenye ulimwengu halisia,hivyo kupunguza makini yao.

vi. Hupisha shughuli inayofuata (k.m utegaji wa vitendawili) iwapo shughuli ya utambaji imekwisha.

vii. Hutuliza hadhira, pengine kwa kuipa suluhisho kwa mgogoro ulipo kwenye ngano. K.m inaweza kuonyesha kuuawa kwa zimwi na kurejeshwa kwa usalaroa katika jamii.

viii. Hutia mshawasha wa kusikiliza ngano nyingine, pengine kupitia taharuki ambayo huenda ikaibuliwa na fani au kukatizwa na msuko wa ngano yenyewe. (za kwanza 4x2=8) 11